

FANI KATIKA NYIMBO TEULE ZA ANASTACIA MUKABWA

MBURU JAMES MUNGAI

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA IDARA YA
KISWAHILI**

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2014

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa na mtu yeyote kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu chochote au taasisi yoyote.

MBURU JAMES MUNGAI

Sahihi

Tarehe.....

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

DKT. Nyachae Michira

(Msimamizi)

Sahihi

Tarehe.....

DKT. Tom Olali

(Msimamizi)

Sahihi

Tarehe.....

TABARUKU

Naitabarukia kazi hii wazazi wangu wapendwa Peter Mburu Mungai na Mary Murugi Makimei kwa kujinyima ili kunilea, kunielimisha na kunihakikishia msingi bora.

Pia nawatabarukia ndugu, dada na marafiki zangu, bila kumsahau mpenzi wangu. Mungu awabariki nyote mliochangia katika ufanisi wa kazi hii.

SHUKRANI

Ningependa kuwashukuru watu wote waliochangia ufanisi wa utafiti huu kwa njia moja au nyingine. Tasnifu hii isingekamilika bila ushauri na usaidizi wao. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya, uhai, uvumilivu, maarifa na hata kunipa rasilimali niliyotumia kugharimia shahada ya uzamili. Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Daktari Tom Olali na Nyachae Michira kwa mawaidha mazuri, ushauri na uelekezi mwema walionipa kila nilipouhitaji. Ushauri wenu wa kitaaluma ulinisaidia kufika mwisho wa safari hii. daima nitaishi kuwakumbuka kwa wema wenu.

Aidha ninawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Isimu na Lugha kwa mchango wao wa ushauri na kunifunza somo la Kiswahili. Mlinionyesha moyo wa wema na hekima na kila mara mlihakikisha nimepata elimu ya kutosha. Mlijitolea mhanga kuhakikisha kuwa masomo yetu yamekamilishwa kwa wakati ufaao.

Ninawashukuru nyote mliotusaidia katika masomo yetu ambao ni pamoja na Prof John Habwe, Prof Abdulaziz, Prof Kyalo Wamitila, Prof Mwenda Mbatia, Prof Kithaka Wa Mberia, Dkt Mukhwana, Prof Kinene Wa Mutiso, Dkt Buregeya, Dkt Zaja Omboga, Dkt Tom Olali, Dkt Amri Swaleh na Basilio Mungania.

Shukrani zangu pia ziwaendee wenzangu wote tuliosoma nao kwa ushirikiano na ukarimu wao. Tumepitia mengi ambayo yalikuwa yakitulia moyo na wakati mwingine tukivunjika moyo kiasi cha kukata tamaa lakini tulihimizana na kusaidiana kwa hali na mali, ili kuhakikisha kuwa hakuna mmoja wetu amelemewa na safari hii. Tuliokuwa nao darasani ni pamoja na Benjamin Kilanga, Ann Njoroge, Ann Raitania, Millicent Aoko, Mary King'ora, Mirianga Kaumeuru na Emaita Karoki. Mungu awabariki.

IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia fani katika nyimbo za Anastacia Mukabwa kwenye albamu yake *kiatu kivue*. Utafiti huu uliongozwa na msingi wa nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza matumizi ya fani katika nyimbo za injili hasa kwa kumrejelea mtunzi Anastacia Mukabwa.

Nyimbo ni mojawapo wa tanzu za fasihi simulizi ambazo zina mwelekeo wa matumizi ya lugha yenye sauti zenye mahadhi na midundo zilizotengwa ili kunasa hisia za hadhira. Nyimbo hunasibika kwa mpangilio maalum wa maneno, vipashio vya kiisimu, mada za kimaudhui, kupitia midundo maalum na ujenzi wa taswira. Nyimbo huwakilisha mawazo, fikra na falsafa ya mtunzi kwa njia inayosababisha changamoto na mawasiliano kwa hadhira lengwa. Kwa hivyo, tuna ushahidi wa kutosha kwamba nyimbo za Kiswahili zina ukwasi mkubwa wa vipengele vya kifani vinavyopaswa kuchunguzwa katika kiwango cha usomi. Utafiti huu ulishughulikia matumizi ya fani kama kipengele cha kisanaa katika kazi ya fasihi, ni kipengele kinachojenga umbo la kazi ya sanaa.

Utafiti huu ulidhihirisha kwamba nyimbo za Anastacia Mukabwa zina ukwasi mkubwa wa fani kama vile wahusika, maudhui, mandhari, toni, tamadhali za semi, sitiari, ishara ,umbo na mtindo

Historia ya Anastacia Mukabwa

Anastacia ni mwimbaji wa nyimbo za injili ambaye umaarufu wake ulipaa zaidi baada ya albamu aliyotoa ya **Kiatu Kivue**. Tofauti na waimbaji wengi wa nyimbo za injili nchini Kenya, Mukabwa hutumia lugha sanifu ya Kiswahili na yenye ufasaha mkubwa, hali iliyowafanya baadhi ya watu kumfikiria kuwa ni Mtanzania. Yamkini ni mwimbaji ambaye kiusuli ametoka katika maisha ya kichochole yaliyomlazimu wakati fulani maishani kuishi kwa kuombaomba mitaani. Katika mahojiano na mtangazaji wa *West FM*, Rosemary Wachiye, Anastacia alisema kuwa maisha yao yalikabiliwa na ndaro nyingi sana baada ya kifo cha baba yao.

Anastacia ni mzawa wa Budalang'i katika Kaunti ya Busia. Masomo yake ya msingi ya upili aliyasomea mjini Mombasa. Ameolewa na ana watoto wawili. Kulingana naye, ndoa yake ina kisa kirefu ambacho kilimchochea kuokoka. Yamkini, mumewe alikuwa Mwislamu na kawaida ya wanaume katika dini hii, aliamua kuoa mke wa pili. Hili lilimhangaisha sana Anastacia hata akaamua kuokoka. Kwa bahati nzuri mumewe alighairi kuoa mke wa pili naye akaokoka vilevile.

Albamu yake ya kwanza ilikuwa *Umenitoa Shimoni*, ambayo haikutambulikana sana kama ilivyofanya ile ya **Kiatu Kivue** aliyomshirikisha mwimbaji Mtanzania Rose Muhando kuimba na ambaye anamtaja kama mlezi wake kimuziki. Hii ya pili, **Kiatu Kivue** ilivuma sana. Na kwa kweli waliomuona Rose Muhando katika video ya albamu hiyo, walidhani kuwa ndiye mtunzi hasa wa nyimbo hizo. Hili hata hivyo Anastacia alilijibu kwa maelezo ya kipekee kuhusu usuli wa kukutana na Muhando na hatimaye kushirikishwa kutoa mchango wake katika santuri hiyo.

“Nilikutana na Rose katika hafla mjini Mombasa muda mrefu uliopita. Baada ya kuimba jukwaani, aliniita kando na kunieleza kuwa Mungu amemwagiza (yeye Rose) kwamba anikuze katika uimbaji wangu na kweli amelitimiza hilo na anazingatia neno lake.” Tafsiri Yangu.

Ni mwimbaji stadi kwa kutumia lugha. Uchunguzi wa nyimbo zake unadhihirisha uwezo wake wa kutumia lugha mbalimbali za ulimwengu. Kwa mfano, anatumia mojawapo ya lahaja za Kiluyia [si lahaja mama na pia lugha ya Kizulu], katika albamu hii *Kiatu Kivue*, kuna wimbo ulioimbwa kwa lugha Kizulu .Wimbo huu unajulikana kama *Zinzilela* na tafsiri yake ni kumwomba Mwenyezi Mungu apokee utukufu kwa sababu hakuna yeyote aliye na uwezo kama wake.

YALIYOMO

UNGAMO.....	i
TABARUKU	ii
SHUKRANI.....	iii
IKISIRI	iv
HISTORIA YA ANASTACIA MUKABWA	v

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Tatizo La Utafiti.....	3
1.3 Madhumuni ya utafiti.....	4
1.4 Nadharia tete	4
1.5 Sababu za kuchagua mada hii.....	5
1.6 Upeo na mipaka ya utafiti.....	5
1.7 Msingi wa kinadharia.....	7
1.7.1 Lugha ya kitamathali na mtindo	8
1.7.2 Uteuzi na mtindo.....	9
1.7.3 Uchimuzi wa mtindo.....	10
1.7.4 Muwala, mshikamano na mtindo	10
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada.....	12
1.9 Mbinu za utafiti.....	14
1.9.1 Sampuli	15
1.9.2 Nyenzo za utafiti	16

SURA YA PILI

UANISHAJI WA NYIMBO

2.1 Maana ya nyimbo.....	17
2.2 Umuhimu wa nyimbo	19
2.3 Aina za nyimbo	20
2.3.1 Bembelezi/Bembe/ Bembezi.....	20
2.3.2 Nyimbo za tohara/nyiso	21
2.3.3 Nyimbo za kazi (hodiya).....	22
2.3.4 Nyimbo za kumpa mtoto jina.....	23
2.3.5 Mbolezi /nyimbo za maafa/tahalili	24
2.3.6 Nyimbo za mapenzi	26
2.3.7 Nyimbo za kisiasa	27
2.3.8 Nyimbo za mashujaa.....	28
2.3.9 Nyimbo za harusi	29
2.3.10 Nyimbo za tambiko.....	29
2.3.11 Nyimbo za sifa	29
2.3.12 Nyimbo za dini.....	31
2.4 Hitimisho.....	31

SURA YA TATU

UFAFANUZI WA FANI KATIKA NYIMBO

3.0 Utangulizi.....	32
3.1 Maana ya Fani.....	32
3.1.1 Fani na maudhui.....	33

3.1.2 Vipengele vya fani	33
3.1.2.1 Lugha	33
3.1.2.1.1 Maana ya lugha	33
3.1.2.1.2 Uteuzi wa msamiati.....	36
3.1.2.2 Mandhari/Mahali.....	37
3.1.2.2.1 Mandhari halisi	37
3.1.2.2.2 Mandhari ya kidhahania.....	37
3.1.2.2.3 Mandhari ya kiishara.....	38
3.1.2.3 Umbo na mtindo	38
3.1.2.4 Ishara.....	39
3.1.2.5 Toni	40
3.1.2.6 Wahusika/uhusika	41
3.1.2.7 Tamathali za usemi	42
3.1.2.7.1. Sitiari.....	42
3.1.2.8.1 Aina za sitiari	43
3.1.2.7.2 Chuku.....	44
3.1.2.7.3 Tasifida	45
3.1.2.7.4 Tashihisi.....	45
3.1.2.7.5 Tashbihi.....	45
3.1.2.7.6 Dhihaka.....	46
3.1.2.14 Takriri	47
3.1.2.7.8 Mdokezo	47
3.1.2.8 Hitimisho.....	47

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA FANI KATIKA NYIMBO ZA ANASTACIA MUKABWA

4.0 Utangulizi.....	48
4.1 Lugha	49
4.1.1 Uteuzi wa msamiati.....	49
4.1.2 Aina ya msamiati	52
4.2 Toni	56
4.3 Mandhari	58
4.4 Wahusika / uhusika.....	59
4.5 Ishara.....	61
4.6 Ploti.....	61
4.7 Wakati.....	64
4.8 Tamathali za Usemi	64
4.8.1 Sitiari.....	64
4.8.2 Takriri	65
4.8.3 Takriri nomino na nomino	66
4.8.4 Takiriri ya kitenzi kitenzi.....	66
4.8.5 Takriri neno.....	67
4.8.6 Takriri kibwagizo.....	67
4.10 Mdokezo	68
4.11 Nidaa.....	69
4.12 Tashtiti	69
4.13 Tashihisi.....	70

4.14 Tasifida	71
---------------------	----

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi.....	72
---------------------	----

5.1 Kuhusu madhumuni ya utafiti.....	72
--------------------------------------	----

5.2 Muhtasari wa matokeo.....	72
-------------------------------	----

5.3 Changamoto tulizokubana nazo katika utafiti.....	75
--	----

5.4 Pendekezo	75
---------------------	----

MAREJEREO	77
------------------------	----

VIAMBATISHO	80
--------------------------	----

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi

Utafiti huu unalenga kuchunguza matumizi ya fani na mbinu nyingine za sanaa katika nyimbo mojawapo wa tanzu za fasihi simulizi. Wataalamu mbalimbali wametoa maelezo mbalimbali kuhusu maana ya fani. Maafikiano ya maelezo kuhusu fani ni kwamba ni vile vipengele vya kisanaa ambavyo kwa pamoja hujenga umbo la kazi ya sanaa. Vipengele hivyo hasa huhusu mtindo wa kipekee wa umbuji na ubunifu wa mwandishi. Kazi ya fasihi hujengwa kutokana na uteuzi wa kibinafsi wa mtunzi ambaye pia huwa na uwasilishaji wa kipekee na wenye kutambulisha ubinafsi wa umbuji huu wake.

Vijielezi mbalimbali vya fani hudhihirisha kwamba umbuji wa kisanaa huwa na upekee kwa kila mtunzi. Hubainisha pia kwamba fani ni mjumuiiko wa vipengele mbalimbali vya kisanaa ambavyo huchangia katika ukamilifu wa kazi maalum. Fani hutazamiwa kuwa ni muumano wa kindani wa viungo vyake na wakati huo huo ikawa inakubaliwa na jamii. Uamilifu wa fani ni kuunganisha viungo mbalimbali na kuzihusisha kwa njia ambayo vinaweza kuchangia katika ukamilifu wa kazi ya sanaa.

Catman (1967: 64) anaelezea kuwa fani ni umbuji kama uteuzi wa kisani wa kibinafsi wa kila mtunzi. Mwandishi huchagua vipengele vyote ambavyo hushirikisha katika kazi yake kwa namna ambayo inaweza kufanikisha malengo anayokusudia. Anaeleza fani kama kaida ya uchaguzi wa mada na jinsi inavyowasilishwa, vile inavyopangiliwa na muundo wake. Fani ni kiungo kinachohusishwa na maudhui, ploti, mpangilio, uhusika na ujumi.

Uteuzi huu unaozunguka dhana ya fani huashiria kwamba mtindo huwa na upekee kwa kila mtunzi kutokana na jinsi anavyoteua na kutumia lugha. Mawazo yake hutokana na ubinafsi wa mtazamo wake kuhusu swala analojadili. Kila mtunzi huwasilisha imani yake kwa njia inayompendeza na kumridhisha. Kwa ufupi, fani ni kitendo cha mtu binafsi. Ni mtindo ambao mtunzi huteua kufidia matakwa ya sanaa na maudhui katika kazi yake. Ni zile mbinu za kisanaa ambazo mtunzi huteua na kutumia katika utunzi na uendelezaji wa kazi yake.

Mbinu anazotumia kisanaa katika uwasilishaji kwa jumla ni fani. Nao upekee wa uteuzi na uwasilishaji wa mbinu hizi ni mtindo. Senkoro (1982:14) anasema kuwa mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hatimaye hutokeza au huonyesha unafsi na upekee wa mtunzi wa kazi fulani mahsus.

Sifa ambazo hutuwezesha kupambana nyimbo au kuchanganua kutoka matawi mengine ya kifasihi ni za kifani zaidi kuliko za kimaudhui. Maudhui ya kisanii ni yaleyale, hayabadiliki na huendelezwa kwa mitindo mbalimbali.

Vipengele vya fani kama lugha, mtindo na wahusika husaidia sana katika uanishi wa tanzu za fasihi. Kwa mfano, lugha inayotumika katika nyimbo ina ukwasi wa tamathali za semi ikilinganishwa na riwaya na tamthilia. Mandhari ploti na toni hutufaa katika ufafanuzi wa nyimbo. Katika kiwango cha lugha vipengele kadhaa huzingatiwa navyo ni msamiati, maana, uwezo na mahusiano na matumizi ya tamathali. Katika kiwango cha kwanza uteuzi wa msamiati, aina ya msamiati na motisha katika matumizi ya msamiati na mazingira ambamo msamiati hutumiwa ili kuibua maana zina athari zake katika tungo.

Kwa hivyo tasnifu hii itahakiki vipengele mbalimbali vya fani kama vinavyojitokeza katika nyimbo za Anastacia Mukabwa.

1.2 Tatizo La Utafiti

Tatizo letu la utafiti limo katika kipengele cha fasihi cha fani. Umili wa fani ni mkubwa sana katika sanaa. Matumizi mazuri ya fani hupendeza na kuvutia katika sanaa. Fani huchukua jukumu la kupitisha ujumbe kama inavyokusudiwa kwa hadhira. Matumizi mabaya ya fani huichakaza kazi na kuathiri mawasiliano. Hali hii haivutii katika sanaa na lazima makini na hadhari kubwa vichukuliwe katika kuhakikisha kwamba matokeo ya matumizi ya fani ni upitishwaji ujumbe kwa njia inayopendeza na uwasilishaji wake kwa mbinu zinazonasa nadhari.

Watafiti na wasomi mbalimbali wa fasihi wanashughulikia tanzu za fasihi simulizi zinazohusishwa na nyimbo kwa kuzingatia maudhui bila kuhakiki fani zinazoambatana na nyimbo. Utafiti huu unachunguza maana ya kimuziki inavyojengeka kwa kutumia fani katika utanzu wa fasihi simulizi.

Kwa msingi huu tutachunguza matumizi ya tamathali na mbinu mbalimbali za sanaa katika nyimbo za Anastacia Mukabwa kama anayetumia lugha kitamathali kuwasilisha ujumbe kisanaa, kwa hadhira lengwa. Nyimbo tulizoteulia kwa utafiti huu ni kama vile *kiatu kivue*, ambao kwa kweli haimaanishi kukivua kiatu bali ni jazanda iliyo na maana fiche. Wimbo wake mwingine *anayekudharau siku moja atakusalima kwa heshima* ni ishara ya kinaya, katika maisha ya binadamu. Hii hata hivyo inaweza kutarajiwa katika matumizi ya sajili yoyote ya kidini. Ujumbe huu unaweza kutazamwa kijuujuu tu hivyo ulivyo lakini ukweli ni kwamba ikichunguza

kwa makini yaliyomo katika kinaya hicho cha maisha inakuwa rahisi sana kujinyenyekeza. Yaani aliye juu anaweza kurudi chini na wa chini akapanda juu kabisa. Kwa hivyo, hakuna haja ya kujipa ndweo bila matarajio ya mkondo huu mwingine wa maisha ambao unaweza kuishia kurudi chini.

Kwa hivyo, tatizo letu limo kwenye aina za fani alizotumia msanii. Ni fani faafu zinazotekeleza majukumu ya umbuji na ubunifu wa kazi ya kifasihi? Ni kutokana na kauli hii ndipo tumeteua kuhakiki matumizi ya fani katika nyimbo za Anastacia Mukabwa kwenye albamu *kiatu kivue*.

1.3 Madhumuni ya utafiti

- i) Kuchunguza matumizi ya fani katika nyimbo za injili za Anastacia Mukabwa.
- ii) Kujadili ufaafu wa fani kama zilivyotumiwa na Anastacia Mukabwa kuwasilisha ujumbe wake katika albamu *Kiatu Kivue*.

1.4 Nadharia tete

Katika utafiti huu tunakusudia kudhihirisha nadharia tete zifuatazo:

- i. Fani za fasihi andishi alizotumia mwimbaji zimeingiliana vyema katika utanzu wa fasihi simulizi
- ii. Msanii Anastacia Mukabwa ametumia fani kwa umakinifu katika nyimbo zake.

1.5 Sababu za kuchagua mada hii

Nyimbo kama mojawapo wa tanzu za fasihi simulizi hazijafanyiwa uchunguzi wa kutosha hasa katika lugha ya Kiswahili. Wengi wetu tunapenda burudani na muziki, lakini inasikitisha kwamba wengi hupungwa na midundo tu bila kuchunguza ujumbe. Maudhui katika tungo ni kigezo cha kimsingi cha kupima ujuzi wa mwimbaji. Maudhui huwasilishwa kwa kutumia fani mbalimbali. Katika tafiti zilizofanywa hapo awali kuhusu nyimbo, tumeonyeshwa kuwa kuna haja, uchunguzi zaidi kufanywa kuhusu suala la nyimbo. Kazi nyingi zilizopo hasa kuhusiana na muziki ulimwenguni. Mara nyingi zimeangazia muziki kwa mtazamo wa wanafunzi wa somo la muziki tu, hivyo mijadala mingi inajikita katika midundo tu bila kuchunguza undani wa ujumbe na fani. Tuna ushahidi wa kutosha kwamba nyimbo za Kiswahili zina ukwasi mkubwa wa vipengele vya fani vinavyopaswa kuchunguzwa katika viwango hivi vya usomi na hata zaidi. Ni kutokana na madai haya tulichagua kutafiti nyimbo za mwimbaji Anastacia Mukabwa aliye na ujuzi mkubwa wa kutumia lugha ya Kiswahili katika uimbaji wake

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Kazi hii inashughulikia uchambuzi wa tamathali na mbinu kadhaa za sanaa katika nyimbo za Anastacia Mukabwa katika albamu yake iliyompa umaarufu zaidi ya *Kiatu kivue*. Ingawa mwelekeo wa uchunguzi huu kulingana na sehemu ya 1.2 inaelekeza kuwa utahusu kijisehemu tu cha fani, vipengele mbalimbali vya fani kama vile uhusika, toni, maudhui, tamathali za semi vitarejelewa. Msokile (1993:57) anaeleza fani kama vipengele vya kisanaa katika kazi ya fasihi. Ni vipengele vinavyojenga umbo la kazi ya sanaa. Kulingana naye, vipengele hivi ni pamoja na muundo, mtindo, mandhari, wahusika na lugha.

Wamitila (2003:190) anazifafanua fani kama mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui katika kazi ya sanaa. Kimsingi, fani ni jumla ya vifaa au vipengele vinavyotazamwa na wahakiki kama nguzo zilizotumiwa na mtunzi wa kazi ya sanaa kuwasilisha maudhui yake. Kwa hivyo, ingawa lengo si kuzungumzia maudhui suala la maudhui, litajipenyeza hapa na pale. Inavyojitokeza katika mawazo yaliyorejelewa kueleza fani hapa, ni dhahiri kwamba fani na maudhui haviwezi kutenganishwa. Hivyo basi, hatutachelea kutaja au kueleza maudhui ya nyimbo hizi katika utafiti huu. Hata hivyo, kwa kiwango kikubwa tutajikita katika kueleza fani.

Aidha, ni muhimu kueleza hapa kwamba kipengele cha fani ni kipana, sana kwa hivyo hatutachambua fani zote bali tutazingatia fani zinazoingiliana na nyimbo..., Vilevile, utafiti huu uliteua kutumia albamu moja ya mtunzi Anastacia Mukabwa. Nyimbo zake ni nyingi na sifa zinazodhihirika katika albamu husika pia zinadhirika katika albamu zake nyingine. Isitoshe, ni mtunzi anayeendelea kuimba, yaani hajastaafu katika taaluma ya uimbaji kwa hivyo haiwezekani kukisia kwamba wingi wa nyimbo zake utafikia mwisho lini; hivyo mtafiti naye akomee hapo katika uchunguzi. Ikumbukwe pia kuwa waimbaji wa nyimbo za injili ni wengi, hivyo isingewezekana kuwashughulikia wote katika mkumbo mmoja tu wa utafiti. Pamoja na wingi wao, wengine huimba katika lugha zisizo za Kiswahili. Utafiti huu unahusu nyimbo za Kiswahili na hivyo basi hata nyimbo za mtunzi na mwimbaji huyu alizoimba katika lugha zisizo za Kiswahili hazitachunguzwa.

1.7 Msingi wa kinadharia

Utafiti huu utaongozwa na nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Tumeichagua nadharia hii kwa sababu itatufaa katika uhakiki wa fani katika nyimbo za Anastacia Mukabwa. Hii nadharia inatuelekeza katika kuchanganua vipengele mbalimbali vya kifani.

Nadharia ya uhakiki wa kimtindo ina historia ndefu iliyofuata mikondo mbalimbali. Barry (2002) ni miongoni mwa wananadharia ambao wamehusika katika uelezaji na ufafanuzi wa historia hii ndefu pamoja na mawazo ya mwelekeo wa kihakiki wa mtindo. Kulingana na mtaalamu huyu wa nadharia, mwelekeo wa kimtindo una mizizi yake katika nadharia ya balagha ya zama za akina Aristotle na Cicero katika jadi ya Uyunani na Urumi Wananadharia ya balagha walithamini na kusisitiza jinsi ya kuzungumza, kupanga mjadala kutoa hotuba na kuwasilisha ujumbe. Wananadharia hawa walijihusisha na ufafanuzi wa matumizi ya lugha katika masimulizi, uteuzi wa maneno, mpangilio wake na namna ya kuunda ruwaza. Aidha walielizea matumizi ya tamathali za usemi na mbinu nyinginezo za kibalagha ili kuleta athari kuu.

Mwelekeo wa kimtindo ulianza kuenea kwa kasi Uingereza na Marekani. Miongoni mwa waliondeleza mawazo ya mwelekeo huu ni Chatman (1967), Leech (1969) na Hillary (1973). Katika awamu hii, mawazo ya mtindo yalitumika katika ufinyu wake kwa kuzingatia vipengele vya kisarufi kama vile vya kifonolia, kimofolojia na kisintaksia.

Katika miaka ya 1980 mwelekeo wa uhakiki wa mtindo ulizidi kubadilika kupanuka na kuanza kuzingatia data nyingine zaidi na isizo za kiisimu. Mabadiliko haya yalichochea na haja ya kuhusisha mawazo ya mwelekeo huu katika uchanganuzi wa tanzu nyinginezo za fasihi. Leech na Short M. (1981:13) wanasema “mtindo ni namna lugha inavyotumiwa katika muktadha na mtu fulani kwa lengo fulani.” Wanasisitiza kuwa katika upana wake, neno mtindo linatumika

kwa usemi wa kisimulizi na maandishi katika maswala ya kifasihi. Hata hivyo, sisi tunajishughulisha na usemi wa kisimulizi kwa njia ya nyimbo. Mtindo unazingatia mambo mengi kiasi kwamba imekuwa vigumu kwa wanafasihi kujua njia moja ya kuieleza dhana hii. Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na jitihada za kuelezea njia mpya katika mwelekeo wa kihakiki wa mtindo. Tutazingatia mwelekeo huu mpya wa uhakiki wa kimtindo. Simpson (2004:21) anaorodhesha na kufafanua mambo ya kimsingi ambayo yanafaa kuchunguzwa katika kazi ya kifasihi na mhakiki ambaye anatumia mwelekeo wa kihakiki wa mtindo. Kulingana na mtalamu huyu, kuna mambo manane ya kimsingi ambayo yanafaa kuchunguzwa katika matini au kazi ya kifasihi kwa kutegemea mwelekeo wa kihakiki wa kimtindo Mambo haya ni;

- (a) Lugha ya kitamathali na mtindo.
- (b) Uteuzi na mtindo.
- (c) Sarufi na mtindo.
- (d) Uchimuzi na mtindo.
- (e) Usimulizi na mtindo.
- (f) Itikadi na mtindo.
- (g) Muwala, mshikamano na mtindo.
- (h) Mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo.

Kwa mjibu wa utafiti huu tutazingatia vipengele vitatu vya uhakiki wa kimtindo ambavyo vina mwingiliano na uhakiki wa fani.

1.7.1 Lugha ya kitamathali na mtindo

Kiwango mojawapo muhimu cha kuchunguza katika mkabala wa uhakiki wa kimtindo na ambacho ndicho kiini cha tasnifu hii ni kiwango cha matumizi ya tamathali za usemi. Mhakiki

anafaa kubainisha mbinu mbalimbali za tamathali zilizotumiwa katika kazi fulani pamoja na kutathmini athari za mbinu hizo. Daraja hii ya mtindo inatokana na sababu kuwa tamathali za usemi huchukua nafasi kubwa na muhimu katika uchunguzi wa lugha ya kifasihi. Tamathali za usemi huwa ni mojawapo ya mbinu za matumizi ya lugha ya mkato ya kisani, na humwezesha mtunzi kusema mengi kwa maneno machache yenye mvuto mguso na mnato. Halman (1986:202) anaeleza kuwa tamathali za usemi ni matumizi mbalimbali ya lugha ambayo hukiuka mtindo uliozoeleka ili kuleta athari au maana fulani. Matumizi ya lugha kwa namna hii huenda kinyume na kile ambacho wazungumzaji wa lugha fulani wanakielewa kuwa kawaida, wastani na yenye mpangilio wenye ruwaza ya maneno. Mfano wa tamathali za usemi ni sitiari, taashira, kijembe, tanakali za sauti, ritifaa, na dhihaka. Kulingana na Simpson (2004: 41), tamathali za usemi ambazo zimepewa nafasi kubwa na wanaumitindo wanaziona tamathali hizi mbili zikihusu ubunifu mkubwa katika uhamishaji wa maana kutoka kwa kitu kimoja hadi kingine katika kazi ya fasihi. Nakubaliana na kauli hii kwa sababu tamathali hizi zimejitokeza bayana katika nyimbo za Anastacia Mukabwa ambazo tutahakiki katika sura ya nne. Tamathali za usemi hazipatikani tu katika fasihi bali hutumika kwa wingi katika mazungumzo ya kila siku.

1.7.2 Uteuzi na mtindo

Mhakiki wa kimtindo anafaa kuzingatia suala la uteuzi katika matumizi ya lugha. Kila mtunzi huwa na uhuru wa kuteua msamiati atakaotumia, lahaja moja kinyume na nyingine, kutumia au kutotumia lafudhi au kutumia sajili. Uteuzi huo unaweza kuwa wa kibinafsi au ukaongozwa na kaida fulani za utunzi au za kitanzu. Msamiati autumiao mtunzi huwa ni mojawapo wa vitambulishi vya matini na vilevile mtunzi wa kazi husika. Ni muhimu kutaja hapa kuwa swala la uteuzi katika fasihi haliishi tu katika uteuzi wa msamiati bali huhusisha vipengele vingine vya

matini kama vile uteuzi wa mada na uteuzi wa mandhari. Simpson (2004:22) anaeleza kuwa kila mtunzi huwa na malighafi ya lugha kadha lakini huteua kutumia mojawapo badala ya nyingine katika miktadha mahususi. Kwa sababu hii uteuzi wa kipengle kimoja kinyume na kingine utakuwa na athari tofauti katika usomaji na ufasiri matini husika na mhakiki wa kimtindo anafaa kuonyesha tofauti hizo.

1.7.3 Uchimuzi wa mtindo

Chapman (1974:48) anaeleza uchimuzi kuwa aina fulani ya ukiushi katika matumizi ya lugha ambao hulenga kukifanya kitu kinachozungumziwa kuwa wazi zaidi. Tunakubaliana na Kazungu (1982) kuwa maelezo hayo ya Chapman yana upungufu fulani kwani uchimuzi hautokani tu na ukiushi katika matumizi ya lugha bali na mbinu au miundo mingineyo ya lugha. Hivyo, uchimuzi unafaa kuelezwa kama matumizi ya lugha kwa namna inayokifanya kitu kinachozungumziwa kutokeza mbele au kuwa wazi zaidi. Uchimuzi unaweza kutokea katika kiwango cha kisintaksia, au kisemantiki. Katika kiwango cha kisintaksia mtunzi huenda akakiuka miundo ya vishazi au virai ilhali katika kiwango cha kisemantiki mtunzi huenda akatumia mbinu kama vile urudiaji wa dhana, sauti au maneno. Aidha kuna uchimuzi wa kimaana au kisemantiki ambapo maneno fulani yanapewa maana tofauti au kutumiwa kwa njia ambayo ni tofauti na ilivyozoeleka. Mfano wa uchimuzi hua unapatikana katika tamathali za usemi.

1.7.4 Muwala, mshikamano na mtindo

Msokile (1998:23) anaelezea muwala kama mbinu mbalimbali za kiisimu ambazo huwezesha maneno ya aya au sentensi kuhusiana na kuugana. Mawazo haya ya Msokile yana maana kuwa

matini za kifasihi zina muwala katika viwango vya vijenzi vya sentensi kama vile maneno , virai na vishazi na vile vile katika viwango zaidi vya sentensi kama vile aya. Muwala huwa na jukumu la kuleta mshikamano wa kazi na kuifanya kuwa na umoja na udhabiti.Ni jukumu la mhakiki kuchanganua na kutathmini namna vijengi mbalimbali vya matini husika vinavyohusiana na kulingana na kukamilishana ili kuleta maana na mantiki inayotarajiwa; hii utakuwa na manufaa katika utafiti wetu.

Kutokana na maelezo hayo ya mtaalamu huyo ni wazi kuwa swala la mtindo katika fasihi ni pana mno, kwa hivyo katika utafiti wetu tumechagua vipengele vinne katika uhakiki wa nyimbo.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003:39), “mtindo ni dhana inayotumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi za kifasihi. “Ni taaluma iliyoko kati ya uchunguzi wa lugha na jinsi lugha inavyotumika katika kazi za kifasihi. Huweza kuhusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi fulani za kifasihi.

Mbatiah (2001:580) anasema mtindo ni jinsi mtunzi wa kazi ya kisanaa anavyotumia lugha kujieleza. Anaendelea kueleza kwamba uchanganuzi wa kazi ya kifasihi kimtindo una mambo kama uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, zilizotumiwa, miundo ya sentensi, aya , beti,na kwamba mtindo hujumuisha vipengele vyote vya lugha.

Wamitila (2003: 145) anadai kuwa dhana ya mtindo hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Anasema kuwa uchunguzi wa mtindo unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya zake na uakifishaji. Kwa muhtasari, nadharia ya kimtindo ni nadharia ambayo inajikita kwenye

uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa, uchunguzi huu wa lugha unapania kubainisha ubunifu uliopo kwenye nyimbo teule za Anastacia Mukabwa katika uelewekeji wa matini na ujumbe uliopo katika nyimbo hizo.

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Kuna watafiti wengi waliojitokeza kushughulikia nyanja hii ya fasihi. Miongoni mwao ni, Kirumbi (1975:3) anadai kuwa “Fani ya nyimbo katika fasihi simulizi ni pana sana na huchukua nafasi kubwa katika maisha ya watu. “Jamii yetu ni jamii iimbayo, na katika kila tukio maishani mwetu bado utakuta watu wanaimba”. Hoja hii ni kweli hasa katika utafiti wetu ambapo tunachunguza matumizi ya tamathali za usemi katika nyimbo za Anastacia Mukabwa.

Matteru (1981:30) anakuu “Nyimbo ni aina ya ushairi unaoimbwa pekee au kuhusishwa na ngoma na pia kucheza na mwimbaji wake,”Nyimbo hutekeleza jukumu maalum katika jamii kwa kukuza utangama miongoni mwa wanajamii. Nyimbo pia hutoa hisia tofauti tofauti kama furaha na huzuni. Anazidi kusema kuwa wimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana ya ujumbe kwa jamii. Nakubaliana na maoni ya Matteru. Utafiti wake umechangia sana kuchanganua fani katika nyimbo za Anastacia Mukabwa.

Yalwala (1991) alitafiti kuhusu maudhui katika nyimbo za John Mwale ambapo alitathmini maudhui hasa mambo yanayoibuka. Maudhui yaliyojadiliwa ni yale ya siasa, umoja, uzalendo na maadili katika jamii. Utafiti huu wa Yalwala ulikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwani katika kujadili fani kipengele cha maudhui kilijitokeza. Nyimbo hizi huibuka kufuatia utaratibu fulani ambao unachangiwa na maswala ibuka katika jamii. Utafiti huu unatofuatiana na wetu kwa

sababu ulishughulikia maudhui ya nyimbo kwa jumla ili hali utafiti wetu unashughulikia fani katika nyimbo za Anastacia Mukabwa.

Wamitila (2002: 70) alisema fani simulizi ni mali ya jamii. Hakuna yeyote katika jamii ambaye anaweza kudai kwamba fani ni yake. Fasihi huwa inapokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hivyo kila jamii ina fasihi simulizi yake tofauti na jamii nyingine, na vizazi hivi ndivyo huhifadhi fasihi hii ili kupokezwa kwa vile vitakavyokuja. Maoni haya yanatuelekeza kufahamu usuli wa nyimbo. Kwa hivyo fasihi simulizi huangazia maswala ya jamii nzima lengwa na sio mtu au aila fulani pekee.

Fasihi simulizi basi ni sanaa ambayo inatumia lugha hasa maneno ambayo yametamkwa kupitia kinywa cha binadamu. Kinoti (2008) anasema fasihi simulizi (nyimbo) ni fasihi-mama, inayo historia ndefu kwani ilianza tu punde binadamu alipoumbwa. Kwa hivyo, fasihi simulizi ni mali ya jamii yenye manufaa mengi kwa binadamu, kupitia uwezo wake binadamu wa kutamka maneno huwasilisha ujumbe kwa njia ya mazungumzo, kughani, uimbaji na kadhalika. Kwa hivyo fasihi simulizi huweza kuelezea hisia za binadamu kama vile furaha, matarajio, kero na pia mila na desturi za jamii husika.

Wamitila (2003:65) anasema nyimbo huwa na mawazo mazito na hutumiwa kuonyesha uhusiano wa jamii, migogoro, kukejeli, kuliwaza, kubembeleza, kutumbuiza, kuongoa na kuburudisha. Anaendelea kusema kwamba takribani shughuli zote za binadamu kama kulima kufuga, kufua, kujenga, kupasha tohara, kuoja, kulea na kuliwaza wakati wa mazishi huandamana na nyimbo

na uimbaji. Maoni ya mtaalamu huyu yamekuwa msingi thabiti wa kuchunguza aina tofauti za nyimbo.

Nkonge (2008) alishughulikia fani na maudhui katika nyimbo za *Joseph Kamaru*. Utafiti wake utakuwa wa manufaa kwa sababu Nkonge alishughulikia maudhui pamoja na fani katika nyimbo zake. Utafiti wake ulidhihirisha kwamba msanii husukumwa na ari ya kueleza matukio ya kijamii na ya kisiasa. Ni bayana kwamba Anastacia Mukabwa ana tajiriba ya kueleza matukio yanayokumba jamii kwa njia ya nyimbo. Kazi hii ya Nkonge imekaribiana na yetu kwani imejadili fani. Kwa hivyo tutanufaika sana na sehemu iliyoshughulikia fani.

Mwisho, katika ufafanuzi wetu kuhusu nyimbo, tutasema kwamba nyimbo ni mawazo yaliyioimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalum. Mawazo hayawezi kutolewa kwa hadhira katika mazungumzo ya kawaida, na yanaleta atharii iliyokusudiwa bali yanahitaji upangaji na umbuji mkubwa na matumizi ya fani ili kufanikisha lengo kwa hadhira. Mawazo ya mwanadamu yanasukumwa na nguvu maalum iliyozingirwa wakati huo na mambo kama furaha, hofu, uchungu, utulivu, na msukumo huu ulimpelekea mwimbaji Anastacia Mukabwa kutoa hisia zake kwa kutunga nyimbo.

1.9 Mbinu za utafiti

Utafiti huu umekuwa wa kushirikisha aina mbili kuu za utafiti. Sehemu fulani ambayo ni pana zaidi imekuwa ya maktabani na nyingine ilikuwa ya nyanjani hasa kwa kumhitaji mtafiti kutambua na kusikiliza nyimbo husika. Kwa kuwa uwanja huu haujaandikiwa sana katika fasihi ya Kiswahili, tulisoma marejeleo mengi ya kazi na lugha nyingine kuu duniani. Hata hivyo, kuna baadhi ya makala muhimu za Kiswahili tulizosoma ili kujenga na kukoleza mtazamo kuhusiana

na aina hii ya fasihi ambayo mtafiti hapa anaiita fasihi ya nyimbo. Kazi hizi tulizosoma zilihusu mada yetu ya utafiti.

Vilevile, tulisoma kazi mbalimbali kuhusu nadharia zinazohusiana na uchunguzi wa kazi ya aina katika fasihi. Mawazo ya wasomi na wananadharia mbalimbali kuhusu nadharia yalikusudiwa kuuongoza utafiti katika misingi ya nadharia. Mawazo haya ni pamoja na yale ya kuzieleza fani mbalimbali ambazo uchunguzi huu ulitazamia kushughulikia. Hizi ni pamoja na sitiari, metumia, uishara, taswira, tashbihi na chuku au udamisi.

Sehemu inayosalia ya data ilipatikana kutokana na kukusanya nyimbo za mwimbaji Anastacia Mukabwa, na kuzichambua kwa vigezo tulivyoweka kwa mujibu wa utafiti huu. Tulirejelea nyimbo tano katika albamu yake ya *Kiatu Kivue*. Hizi ni: ***Kiatu Kivue, Mungu atukuzwe, Wanaokudharau, Manamba wa matatu na Zinzilela***. Ingawa wimbo huu una jina la *Kizulu*, katika data ya Kiswahili katika wimbo huu. kwa hivyo utafiti wetu uliuzingatia ujumbe huo na data ya Kiswahili katika kuushughulia. Kwa hivyo, zoezi lilikuwa kuzikusanya nyimbo hizo, kusikiliza albamu nzima na kuteua baadhi ya nyimbo zilizoonekana kama zinazozingatia madhumuni ya utafiti huu pamoja na upeo wa utafiti wenyewe. Tulitoa sehemu kubwa ya data inayokidhi jumla ya malengo yetu katika utafiti huu.

1. 9.1 Sampuli

Sampuli yetu imetoka katika nyimbo za kidini za msanii Anastacia Mukabwa. Sampuli tuliyotumia ilikuwa sampuli lengwa. Nyimbo za kidini ni nyingi lakini tulichagua nyimbo za Anastacia ambazo zimeimbwa na watu wengi kwa muda mrefu. Nyimbo zingine za kidini zina

mtindo na maudhui yanayofanana na hizi nyimbo, kwa hivyo nyimbo hizi zimewakilisha zote za kidini.

1.9.2 Nyenzo za utafiti

Nyimbo zimekuwa sehemu muhimu sana ya fasihi tangu zamani. Aghalabu kila jamii ina nyimbo zake ambazo hutumiwa kuwasilisha ujumbe fulani kwa jamii. Nyimbo ni sehemu ya utamaduni. Jinsi utamaduni wa jamii fulani ulivyo mpana ndivyo utamaduni huo ulivyo na nyimbo nyingi. Nyimbo zimetungwa kuhusu kila nyanja ya maisha ambapo kuna nyimbo kuhusu ndoa, mapenzi, shughuli za kilimo, dini, kifo na kadhalika.

SURA YA PILI

UANISHAJI WA NYIMBO

2.1 Maana ya nyimbo

Wataalamu mbalimbali wametoa maelezo mbalimbali kuhusu maana ya nyimbo. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Tuki 1981) wimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Naye M'Ngaruthi (2008:41) anasema kuwa nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya kuvutia na kwa mahadhi ya kupendeza. Inabainika wazi kuwa nyimbo zimekuwemo miongoni mwa binadamu hata kabla ya maandishi kuvumbuliwa na imekuwa ni mojawapo wa njia za watu kujitumbuiza katika sherehe mbalimbali ambapo yaaminika binadamu asiyevitika na wimbo au mdundo wa aina yoyote ana kasoro kubwa. Nyimbo vile vile hutumiwa kupitisha ujumbe kwa watu wenye umri tofauti katika jamii. Vile vile Matteru (1981:38) katika makala yake, fasihi simulizi na andishi anasema kwamba nyimbo ni aina ya ushairi unaoimbwa pekee au kwa kuhusishwa na ngoma au pia kwa kucheza na mwimbaji wake pia anadokeza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo na muwala. Wimbo unaweza kuimbwa na mtu mmoja pekee au na wazumi wake wakiifikia mikarara. Vile vile nyimbo zina mfuatano au mpangilio wa sauti mwendo, picha au ishara.

Thonya (1978:80) anasema kwamba wimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana ya ujumbe kwa jamii. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa inabainika kwamba nyimbo ni fani ya fasihi simulizi. Fani hii hutolewa katika muktadha fulani ili maana ieleweke. Inabainika kuwa maelezo haya basi yanatutolea msingi dhabiti wa kuchanganua nyimbo za kidini za Anastacia. Mukabwa, kwenya albamu yake *kiatu kivue*,

Wamitila (2003:103) anasema kwamba wimbo ni kile kinachoimbwa. Anatoa sifa kadhaa za wimbo kama ifuatavyo;

- i) Sauti ya mwimbaji.
- ii) Ala au vyombo vya muziki (ingawa sio lazima.
- iii) Matini au maneno yanayoimbwa.
- iv) Hadhira inayoimbiwa.
- v) Mukadha uliofungamana na wimbo huo kwa mfano ibada, sherehe, kilio na kadhalika.

Wamitila (2013:104) anaendeleza mawazo hayo kwa kusisitiza kwamba kazi ya kisanaa ya nyimbo hutokana na mazingira. Mazingira ndiyo yanayozalisha hisia na hatimaye kwa msanii. Hivyo basi, katika nyimbo panapaswa kuwa na wazo maalum ambalo linawasilishwa kwa hadhira husika kwa njia ya sauti. Wimbo ni tunzu la kishairi linaloimbwa kwa muwala fulani. Ala za muziki zinazotumika huchukua kipaumbele zaidi ya maneno katika wimbo huo.

Umaarufu wa muziki katika wimbo huruhusu maana ya maneno kuchukuliwa sawa na uimbaji wa muziki. Nyimbo ni zao la shughuli za binadamu na hisia zake na hivyo huzingatia miktadha mbalimbali. Nyimbo kuwa zimefunganishwa na mukadha fulani pale ambapo pana hadhira na matini. Hadhira huwa ni wale wanaosikiliza au kuzitazama nyimbo hizi, nayo matini yakiwa ni yale matamshi yenyewe kwa njia ya uimbaji.

Nyimbo ni aina ya tanzu za fasihi simlizi. Fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia lugha, hasa maneno ambayo yametamkwa kupitia kinywa cha binadamu. Nyimbo ni mali za jamii

mbalimbali zenye manufaa mengi kwa biadamu na kupitia uwezo wake wa kutamka maneno huwasilisha ujumbe kwa njia ya mazungumzo, kughani na kuimba.

Kwa hivyo nyimbo huweza kueleza hisia za binadamu kama vile furaha, kero, matarajio, uzito wa fikira na hata matumaini yake pia hueleza imani, mila na hali tofauti maishani.

Nyimbo zapaswa kuwa na mpangilio maalumu na zinapoimbwa hutumia vipengele vingi katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira lengwa. Vipengele hivi ni pamoja na vidokezo, miguno, toni, vituo, kiimbo, kimya kiasi na kadhalika.

2.2 Umuhimu wa nyimbo

Wamitila (2003: 109) anasema nyimbo zina umuhimu katika jamii za Waafrika kwa sababu hutambulisha jamii kwa kusawiri shughuli na maisha ya jamii iliyozibuni. Kwa mfano, nyimbo kutoka jamii ya uvuvi, zitasheheni msamiati unaohusu shughuli za kuvua kama vile majarife., ndoana , dau, para na kadhalika. Nyimbo humwezesha binadamu kutoa hisia zake na pia kujutia kosa alilofanya, mapenzi ama huzuni. Mbolezi humsaidia mtu aliyeathiriwa kutoa hisia za huzuni.

Nyimbo ni njia mojawapo ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii. Rekodi za matukio muhimu katika jamii huhifadhiwa kwa nyimbo na kupokezwa kwa vizazi. Nyimbo hutumiwa kama burudani, kustarehesha na kulisimua. Aidha nyimbo hutumiwa kupitisha amali na mambo ambayo jamii inayathamini. Amali hizo kurekodiwa katika nyimbo mbalimbali kama vile za kazi na kurithishwa vizazi vya jamii hiyo. Mawaidha na thamani za jamii hukaririwa katika nyimbo.

Nyimbo hutumika kuhamasisha watu na kuchochea hisia za kuchangamkia jambo fulani. Nyimbo za kisiasa kwa mfano, huweza kuchochea hisia za kuugana pamoja kutetea haki au kuunga mkono jambo fulani. Nyimbo huakisi ukwasi wa tamaduni na jamii licha ya ukuwaji wa maadili na kuacha mila miongoni mwa vizazi vya leo, nyimbo huchangia majukumu muhimu ya kushauri kuonga, kukejelli, kutia moyo, kuelimisha na kubezi. Basi kwa kubainisha majukumu haya, tutaeleza nafasi ya aina tofauti za nyimbo katika jamii.

2.3 Aina za nyimbo

Kutokana na maelezo na majukumu ya nyimbo tuliyotangulia kuyajadili, ni wazi kuwa kuna aina nyingi za nyimbo. Baadhi ya nyimbo ambazo hupatikana katika jamii za Kiafrika ni :

2.3.1 Bembelezi/Bembe/ Bembezi

Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa ili kuwabembeleza watoto wachanga walale. Nyimbo hizi huimbwa kwa sauti nyororo na mahadhi ya chini walezi au wazazi wa watoto hutumia zao. Nyimbo bembelezi huwa ni fupi na hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kulingana na thamani za jamii hiyo. Nyimbo hizi huimbwa kwa kurudiarudia maneno au kibwagizo.

Mfano: Jamii ya Waswahili

Howa mwana

*Howa mwana, nyamma silie
Macholiyo weka sinife
Watu waje wakushikilie
Howa mwana nyamaa silie:
usilie sinisumbukie
Uyatima wazee wafie
Cheka mwana vilio vishie*

Wimbo huu huimbwa na jamii ya Waswahili. Wimbo huu huimbwa kwa sauti nzuri na mahadhi yenye kupendeza masikio ya mtoto mchanga. Vile vile katika ujumla huu kuna nyimbo

zinazoimbwa na watoto wadogo kwenye shule za malezi na zinazojulikana kama nyimbo za chekecheo! Hizi huhusisha mchezo fulani wa sauti. Zipo nyimbo nyingi ambazo watoto huziimba wakati wa michezo yao. Nyimbo hizi huwa hazina maneno maalumu, hutegemea mwimbaji, mahali, tukio, umri wa mtoto au jinsia yake. Kwa mfano;

Watoto wangu ee
Watoto wangu ee
Eee
Mimi mama yenu
Eee
Sina nguvu tena Eee
Za kuua simba
Eee
Akaua baba akaua mama
Watoto wangu njooni

2.3.2 Nyimbo za tohara/nyiso

Jamii nyingi za kiafrika zilithamini tohara za wavulana na wasichana, ambapo wavulana walikuwa jandoni ilhadi wasichana unyagoni. Nyimbo za tohara husititiza umuhimu wa tohara na kuhitimu kuwa mtu mzima. Wamitila (2003: 122) anasema. “nyimbo hizi hutumiwa kumjuzua mwanajamii matarajio ya jamii kuonya, kumpa maelezo, kimshajilisha na kumwingiza katika tabaka au kundi fulani la kijamii. Tuna kubaliana na kauli hii kwa sababu maudhui ya nyimbo hizi hujikita katika kuwashauri na kuwahimiza vijana kujivunia na kufurahia tohara.

Nyimbo za tohara ziliimbwa kwa malengo tofauti kama vile:

- i) Kuwakusanya pamoja na kuwapa moyo watahiriwa.
- ii) Kuwakebehi wenye uoga.
- iii) Kuwatayarisha watahiriwa ki-hisia ili kukabiliana na kisu kijasiri.
- iv) Kusisitiza majukumu yajayo.

- v) Kuwaandaa wanaohusika kwa majukumu ya utu uzima.
- vi) Kushangilia na kufurahia hatua ya kutoka utotoni hadi utu uzima.

Mfano wa nyimbo za tohara

Ewe kilizi

*Ewe kilizi uliyezoea kujiticha
Nyuma ya mama kujikinga,
dhidi ya milio ya radi iliyo juu mbinguni
Jua kesho ni siku ya siku,
siku ya kujua mbivu na mbichi
Kutafautisha jogoo na vipora,
ngariba taposhika, chake kijembe.
Ndipo utakapojua bayana ukoo wetu si wa kunguru.
Ikiwa hutayari, kisu kukidhihaki
Sithubutu kamwe, uwanjani kunigia
Sijahuniabisha mie, amiyo na akraba nzima.*

Asili: Jamii ya Wakikuyu

Mtunzi hajulikani.

2.3.3 Nyimbo za kazi (hodiya)

Kila jamii ina nyimbo za kazi. Mwafrika kwa jumla huithamini kazi na kukejeli uvivu. Wakati kazi tofauti zinafanywa. Nyimbo huimbwa ili kupitisha muda, kuifurahia kazi, kuondoa uchovu, kutolea maadili na kwa jumla kurahisisha kazi. Kulingana na Wamitila (2003: 118) nyimbo za kazi zina baadhi ya sifa zifuatazo:

- i. Takriri – Maneno na sauti zinazorudiwarudiwa ili kuoana vilivyo na mdundo wa kazi inayoendelea – pia pana tanakali za sauti.
- ii. Maneno mepesi yaliyo rahisi kujifunza na kuimba palepale.

- iii. Maneno, sauti na milio isiyo na maana mradi iweze kujenga mdundo wa nyimbo.
- iv. Kupokezana – kiongozi wa wimbo kupokezana wimbo na wenzake.
- v. Madoido na vigelegele ili kufanya wimbo kuvutia.

Msamiati, wahusika na maudhui katika nyimbo za kazi hutegemea aina ya wimbo, karibu kila kazi wanayofanya watu huwa na nyimbo zake. Kwa mfano kutwanga, kupepetu, uvuvi, uchuuzi na kusuka kazi zinaweza kuwa za nje ama za nyumbani.

Wimbo wa kazi

*Mwongozaji wacha nitwange
Bila ya hakika kama (n) itajaza
Kibuyu cha pombe ichachukayo
Kipokeo: loo, loo!*

*Mwongozaji: twanga bila ya kutikisika na kuyumbayumba,
usikiapo mtikisiko na myumboyumbo inanywewa kipokeo: loo, loo!*

*Mwongozaji: Miwa ya kapera mkuu itavunjika
Kapera mkuu itavunjika
Pingiti zake kama kuni
(haitpondaka vyema)
Kipokeo: loo, loo!*

2.3.4 Nyimbo za kumpa mtoto jina

Jamii tofauti ziliwapa watoto majina kulingana na jinsia ya mtoto huyo. Kuna jamii zilizotumia misimu tofauti kuwapa watoto majina, wengine walipata majina kutegemea majira ya siku au mwaka. Baadhi ya jamii pia ziliwapatia watoto majina kulingana na jinsia. Katika jamii ya Waluo, kwa mfano jina, Atieno (msichana aliyezaliwa usiku (Otieno) mvulana aliyezaliwa mchana. Kuna jamii zingine ziliwapa watoto majina ya wanyama au miti. Jamii kama Agikuyu

walipeana majina kwa watoto wao kutokana na babu, nyanya, mjomba, au shangazi. Nyimbo zilizotungwa na kuimbwa katika sherehe hizi ziliwasifu watu waliotajwa.

Jamii ya Agikuyu

Kahii gaitu maritati

Gaguthi ruhii

Ngwikire ritwa

ii ii ii ngwikire i namba x 2

I ndakwira ukarira i ka maritati

Gwakia rukiiri ugekirwa i ritwa

ii ii ii ngwikire i namba x 2

Ni narua na fuju ka maritati

Gwakia rukiirie ugekirwa ritwa

ii ii ii ngwikire i namba x 2

Tafsiri

1) *Kijana wetu maridadi*

Kesho naije

Nitakutia Jina

Ndio nitakutia jina x 2

2) *Kijana maridadi usilie*

na ije kesho utapewa jina,

ndio utaitwa jina x 2

2.3.5 Mbolezi /nyimbo za maafa/tahalili

Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa wakati wa maombolezi au kilio au katika hafla ya kuadhimisha makumbusho ya mtu aliyefariki, Mbolezi hutofautiana kutokana na jamii kuhusu kifo pamoja na hadhi ya aliyekufa. Kwa kawaida, mbolezi hutoa sifa nzuri za aliyekufa. Katika baadhi ya tamaduni nyimbo hizi hazitumiki tu kuomboleza bali kulalamikia asili ya kifo hicho. Baadhi ya nyimbo hutungwa kusifu marehemu kwa wema aliotenda akiwa hai na kuwatolea changamoto waliobaki kuuiga wema wake na vile vile kuwafariji waliofiwa. Katika kuimba nyimbo za

mbolezi nyimbo za dini pia huimbwa kuwafahamisha watu kuwa kifo ni mapenzi ya mungu, na kila mmoja atapitia njia hiyo. Nyimbo za matanga pia hutegemea umri na umashuhuri wa marehemu. Watu mashuhuri hutungiwa nyimbo maalum na baadhi ya nyimbo hizo hubaki kuwa kumbukumbu kwa muda mrefu.

Mfano 1: Mbolezi ya kijaluo,

Yawa nyonuru wo, wo ngonuru loo

Loo jajuok

Loo jajuok

Lo otero Jaramogi jabondo

Nyonuru loo

Loo jajuok

Loo otero mbuya moja Rusinga

Nyanuru loo

Loo jajuok

Loo otero wuod seda ouko mane wageno

Loo

Loo Jajuok

Tafsiri ya Kiswahili

Jamani kanyageni mchanga, mchanga kangangeni

Mchanga mchawi

Mchanga mchawi

Mchanga ulimtwaa jaramogi wa Bondo

Kanyageni mchanga

Mchanga mchawi

Mchanga ulimpeleka Mboya wa Rusinga

Kanyageni mchanga

Mchanga mchawi

Mchanga ulimtwaa Ouko, Kijana wa Seda

Aliyekuwa tegemeo kuu

Mchanga

Mchanga mchawi

2.3.6 Nyimbo za mapenzi

M'ngaruthi (2008) anasema kuwa mapenzi ni hisia nzito isiyoweza kuelezeka kikamilifu kwa maneno au lugha yoyote. Nyimbo hizi za mapenzi huimbwa kwa matumizi ya lugha iliyojaa ufund, umbuji na hisia za hali ya juu. Hisia hizi zinaweza kuwa za kufurahisha kwa mfano, kwa mwimbaji anayemsifu mpenzi wake au za kusikitisha kwa mpenzi aliyeachwa na mpenzi wake. Ujumbe wa nyimbo hizi hutegemea waimbaji binafsi, umri wao, jinsia, mazingira muktadha na tukio. Nyimbo hizi zinapoimbwa wahusika hudhihirisha hisia zao kwa kutabasamu, kucheka au hata kutokwa na machozi, hasa kwa wale waliosalitiwa na wapenzi wao. Baadhi ya nyimbo hutungwa kwa namna ambazo zinakuza usemezano fulani kati ya mwimbaji na mlengwa, yaani huwa na sifa tunayoita mwito na mwitiko

Mfano: Wimbo wa mapenzi

*Malaika, nakupenda malaika
Nami nifanyeje, kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina we
Ningekuoa malaika*

*Pesa, zasumbua roho yangu
Ningekuoa we dada
Nashindwa na mali sina we
Ningekuoa malaika
Mtunzi Fadhili William
(mdawida) Taxi Driva*

*Taksi driva nikomboleshe,
gari niende Nakuru
Nikamuone Hannah
Aliniahidi nifike Jumamosi*

*Nami sitaki kuvunja promisi
Niliondoka na yule dereva
Tulipofika kule Niavasha
Gari letu lilipata panchari
Ikawa lazima tutachelewa*

*Tulipofika kule Nakuru
Nilimkuta my baby amekasirika
Niliwambia siyo makosa yangu baby
Gali letu lilipata panchari*

*Hiyo promisi ya gari si nzuri
Kwa sababu gari haliaminiki
Kusema kweli gari si kama mtu
Anaekwenda kwa nguvu za damu*

2.3.7 Nyimbo za kisiasa

Nyimbo hizi za kizalendo, huonyesha mapenzi makuu aliyonayo mtu kwa nchi. Pia hulenga kuwashawishi watu kisiasa au hata kuwakosoa na kuwanyumbua wanasiasa kwa matendo fulani.

Wimbo wa taifa ni mfano mzuri wa nyimbo za kizalendo.

Nyimbo za kisiasa zaweza kugawanywa katika viungo vitatu: Nyimbo za kupinga uonevu katika jamii, nyimbo za kuihamasisha jamii kisiasa na nyimbo za kueneza kasumba au mawazo fulani, ili watu wakubaliane na mwelekeo fulani.

Mfano: Wimbo wa taifa (Kenya)

*Eee Mungu nguvu yetu
Ilete baraka kwetu
Haki iwe ngao na mlinzi
Na tukae na uhuru
Amani na umoja
Raha tupate na ustwawi.*

*Natujenge taifa letu
Ee ndiyo wajibu wetu
Kenya istahili heshima
Tuungane mikono
Pamoja kazini kila
Siku tuwe na shukrani*

*Amkeni ndugu zetu
Tufanye sote bidii
Nasi tujitoe kwa nguvu
Nchi yetu ya Kenya
Tunayoipenda
Tuwe tayari kuilindaa.*

2.3.8 Nyimbo za mashujaa

Nyimbo hizi ziliimbwa nyakati za kupigania uhuru na mataifa mbalimbali ya kiasia. Katika jamii za kiasia, wakati mwingine palitokea vita, hivyo kuna watu walioongoza katika kupigana vita, hivi, hatimaye kuibuka washindi. Watu hawa waliteuliwa kuwa mashujaa katika jamii hizi na kutungiwa nyimbo za kuwasifu. M'ngaruthi (2008:42) anasema kuwa baadhi ya nyimbo hizi ziliimbwa kwa malengo kama vile kuwakashifu, wasaliti na kuwasifu mashujaa, kuwatisha maadui, kushangilia ushindi na kutia moyo. Vile Vile ziliimbwa na mashujaa kuwaombea wanalioenda vitani kabla hawajaondoka na kuhifadhi kumbukumbu za yaliyotendeka nyakati za vita, katika jamii mbalimbali, nyimbo za mashujaa zilitumika kuwasifu viongozi wa kijamii. Mfano wa viongozi walioimbiwa nyimbo za mashujaa nchini Kenya ni Mzee Jomo Kenyatta, Arap Moi, Jaramogi Odinga, Dedan Kimathi na wengine.

Nyimbo za mashujaa

*Sifa zake zilitangaa
Zilivuka mabonde na milima kuzagaa
Watu waliozisikia wakashangaa
Wakapigwa hata na butwaa*

*Kitendo alichofanya hakina hata mithuli
Ni Jasiri asiye mfano na imara mno jabali
Aliyepambana kitendo kikubwa akawa hana mwali
Uliongoza mwanya mkuu kila mahali*

*Kisoi wa Munyao kakwea mlima usiokwewa
Kisol wa Munyao katenda makubwa mfano yasiyokuwa
Kaukwea mlima Kenya
Kaukwea mlima Kenya
Lileleni bendera kasimika
Kuwajibisha wote, hii ni nchi huru
(mtunzi hajulikani)*

2.3.9 Nyimbo za harusi

Ndoa ni sherehe muhimu ya kitamaduni katika jamii zetu. Sherehe hii huandamana na kila aina ya tafrija zikiwepo nyimbo. Nyimbo hizi hutumiwa kutoa mawaidha ya ujumbe kwa maarusi wapya, pamoja na matarajo ya jamii na majukumu ya maarusi, vile vile, huwasifu maarusi na wazazi wao.

Nyimbo hizi pia huimbwa wakati wa kuwasindikiza wachumba kabla ya kufunga ndoa kanisani na kupokezana kwa zamu. Kwa jumla nyimbo za harusi huonyesha furaha na wakati mwingine masikitiko kwa upande wa jamii ya msichana.

2.3.10 Nyimbo za tambiko

Wafrika katika asili yao, waliamini Mungu na miungu, hivyo palipotokea janga au tatizo lolote palikuwa na haja ya kufanya tambiko. Wakati tambiko ilikuwa ikifanywa, nyimbo mbalimbali za kumsihi Mungu na miungu ziliimbwa. Nyimbo hizi zilidhamiriwa kuonyesha mshikamano wa jamii husika na pia unyenyekevu wa Mungu. Jamii ya Wakikuyu ilijitolea kutoa dhabibu kwa Mungu (Mulungu) ili awape mvua ya kujikimu pamoja na mifugo yao katika Mlima Kenya.

2.3.11 Nyimbo za sifa

Nyimbo za sifa pia huitwa sifo. Ni nyimbo ambazo hutoa sifa za mtu fulani na michango na mafanikio ya watu katika jamii. Sifo husifu na kutukuza watu ambao wanafanya jambo fulani. Kwa mfano, husifu maarusi, viongozi wa kisiasa, kiuchumi, na kijamii. Nyimbo hizi hutumia sitiari kwa ufundi mkubwa ili kuwanufaisha wanaosifiwa na wanyama ili kuonyesha sifa fulani bia. Kiongozi anaweza kufananishwa na samba ili kuonyesha ujasiri wake. Pia sifa huakisi thamani ya jamii husika. Kila jamii ina thamani yake. Kuna jamii zinazothamini ujasiri wa kivita, nyingine usuli mwema au nasaba tukufu, ufugaji wa mifugo au kilimo.

Utenzi wa Fumo liyongo (jamii ya Waswahili)

*Hadithi niwandikiye
Ya ajabu musikiye
Yalojiri amriye
Mupate kufahamiya*

*Niweleze kwa utungo
Hadithi yake liyongo
Niweleze na mazingo
Mambo yalomzingiya*

*Liyongo kitakamli
Akabaligui rijali
Akawa mtu wa kweli
Na haiba kaongeya*

*Kimo kawa mtukufu
Mpona sana mrefu
Majimboni ya maarufu
Watu huya kwangalia*

Mfano (2) (wimbo wa sifa),

*Sifa zake zilitangaa,
Zilivuka mabonde na milima kuzayaa
Watu waliozisikia wakashangaa
Wakapigwa hata na butwaa*

*Kitendo alichofanya hakina hata mithali
Ni jasiri asiye mfano na Imara mno jabali
Aliyepambana na dhiki za baridi kali
Kufanya kitendo kikubwa akawa kama mwali
Ulioangaza mwanga mkuu kila mahali*

*Kisoi wa Munyao kakwea mlima usiokwewa
Kisoi wa Munyao katenda makubwa mfano yasiyokuwa
Kaukwea mlima Kenya
Kaukwea bendera kasimika
Ku wajulisha wote, hii ni nchi huru,*

2.3.12 Nyimbo za dini

Hizi ni nyimbo ambazo zina uhusiano na Mungu au miungu. Misingi yazo huwa ni ya dini za kienyeji au zile za kimagharibi na nyimbo hizi zinaweza kuimbwa na mtu binafsi au makundi ya watu. Nyimbo hizi hunuia kuwaelekeza watu katika jamii kwa kuwaonya au kuwatia moyo baada ya matatizo fulani kutokea. Mwimbaji anaweza kutumia lugha kwa ufundi akirejelea tamathali za usemi kama methali, mafumbo, na hata semi tofauti katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira tofauti. Nyimbo hizi huimbwa katika miktadha tofauti kama vile; matanga, harusi, kanisani na waimbaji kwa hadhira. Nyimbo za dini huimbwa kwa unyenyekevu ili kumtukua Mungu.

Mfano

*Muumbaji mfalme vitu vyote vyako,
Ni kwa ukarimu wako nina barikiwa
Ni kwa ukarimu wako nina barikiwaa.*

*Uliyeniumba naja kwako leo,
Sina budi kukusifu kwani uliniumba
Sina budi kukusifu kwani uliniumbaa*

*Naja kwako leo kwa upendo
Sifa na shukrani ni kwako leo
Upendo wako wa haki moyo wa shukran
Upendo wako haki moyo wa shukrani*

2.4 Hitimisho

Nyimbo zina historia ndefu katika jamii zetu. Binadamu amekua akitoa hisia zake, uchungu, kero au hata furaha kwa njia ya nyimbo. Hii ni njia yenye mkokoteto mkubwa wa lile lile na inayoacha athari kubwa kwa wasikilizaji. Kila shughuli zetu huambatana na uimbaji kuanzia kuzaliwa, kufuga, kulima, kuvuna, kunywa pombe, kuomboleza hadi kuzika. Nyimbo huchukua maudhui tofauti kutegemea mambo yafuatayo: umri wa hadhira, jinsia, wakati na mandhari. . Vile vile msamiati wake na matumizi ya tamathali kwa ujumla hutegemea fanani na hadhira.

SURA YA TATU

UFAFANUZI WA FANI KATIKA NYIMBO

3.0 Utangulizi

Usimulizi wowote wa kazi ya kifasihi hutegemea lugha kwa kiasi kikubwa. Lugha ndiyo nyenzo kuu ya sanaa ya fasihi. Kwa misingi hii, uchanganuzi wa nyimbo lazima umulike jinsi lugha inavyotumiwa. Usemi unaopatikana katika nyimbo unaweza kuwasilishwa kwa njia kadhaa. Njia kuu ni maelezo ambapo ujumbe unaelezwa au kusimuliwa kwa njia wazi na kinyume chake ni pale ambapo lugha inawasilishwa kwa njia isiyo wazi. Kazi ya fasihi hujengwa kutokana na uteuzi wa kibinafsi wa mtunzi ambaye pia huwa na uwasilishaji wa kipekee na wenye kutambulisha ubinafsi wa umbuji wake. Kwa hivyo, katika sura hii tumejadili uchanganuzi wa fani katika nyimbo.

3.1 Maana ya fani

Madumula (2009: 120) anasema kwamba fani inajumuisha umbo, ufundi na mtindo wa kazi ya sanaa, mambo kama lugha itumikayo, mtindo na mandhari. Naye Kimani na Chimerah (2011:90) wanapoeleza maana ya fani wanasema kuwa “Ushairi ni kongamano la fani, maudhui na muktadha wa kijamii; Fani ndiyo inayobeba maudhui na vipengele muhimu vya fani katika nyimbo ni lugha, muundo, wahusika na mtindo. Kulingana na Wamitila (2008: 345). fani ni jumla ya nyenzo zinazotumiwa kuwasilisha maudhui. Maudhui hayawezi kumfikia msomaji bila ya kuwepo kwa fani ambayo ni njia kuu ya kuwasilishwa kwa maudhui hayo. Tunaweza kujumuisha na kusema kwamba fani ni mjumuiiko wa vipengele vya kisanaa ambavyo huwasilishwa na umbuji ulio na upekee kwa mtunzi maalum.

3.1.1 Fani na maudhui

Kulingana na Wamitila (2008:521)maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi. Maudhui hujumulisha dhamira itikadi, msimamo, maadili, mafunzo na falsafa. Kwa hivyo, maudhui au yaliyomo katika nyimbo hayawezi kumfikia msikilizaji bila kuwepo na nyenzo za kupitisha au kuyawasilisha. Uhusiano uliopo basi kati ya fani au maudhui ni wa kutegemeana, bila fani maudhui hayapo na maudhi nayo hayawezi kuwasilishwa bila kuwepo kwa fani.Uhusiano uliopo kati ya dhana hizi mbili ni muhimu kiasi kwamba fani inaweza kuhusishwa moja kwa moja na ujumbe au maudhui yenyewe. Ni rahisi kusema kuwa fani ni ujumbe.

3.1.2 Vipengele vya fani

Sehemu hii ilichunguza vipengele vinavyounda fani baadhi ya vipengele hivyo ni mandhari, lugha, toni tamathali za usemi, taswira, taashira, ishara, jazanda, na kadhalika.’

3.1.2.1 Lugha

3.1.2.1.1 Maana ya lugha

Wanafasihi na wanalugha wanaelekea kukubaliana kuhusu maana ya lugha. Yafuatayo ni baadhi ya maelezo yao.

Senkoro, F.E.M.K (1982:13) anasema kuwa kipengele cha lugha ni muhimu sana kwani ndicho kinachotofautisha fasihi na sanaa zinginezo. Kwa mfano , kipengele cha muhimu cha uchoraji ni kalamu, rangi na kipande cha karatasi au nguo. Lugha basi ndio njia aitumiayo msanii wa fasihi kuyaeleza mambo mbalimbali ya jamii yake kwa njia ya ubunaji au kusanii. Naye Msokile , (1993:35), anasema kuwa lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana na ambao

hutumiwa na watu wa taifa au kabila moja kwa ajili ya kuwasiliana ni maneno, matumizi yake na mtindo anaotumia mtu kujieleza.

Kwa kuzingatia maoni haya tunaweza kuelezea lugha kama zao la jamii linalotumia maneno au sauti kwa utaratibu maalum unaokubalika katika kuleta mawasiliano na huwa yenye uwezo wa kubadilika kiwakati.

Lugha hutumiwa na wanajamii katika kupashana habari na kuwasiliana. Matumizi yake huwa mengi nahutegemea mahali na hali ya wanaoitumia. Kila mtu au kundi la wanajamii huitumia kivyake, na hivyo kunatokea aina fulani ya matumizi katika fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia. Ina sifa ya kubadilikabadilika na hivyo ni muhimu kuhakiki mabadiliko hayo na athari zake katika lugha kwa jumla.

Uhakiki wa lugha ni muhimu katika kutupa uamili wake na udhibiti wake wa mawasiliano. Waimbaji mbalimbali hutofautiana katika matumizi ya lugha. Hili likitegemea makini yao katika utunzi, tajiriba zao za kuitumia na uwezo walio nao wa kuelezea mambo. Kunga wanazozitumia za lugha na uhusiano wake wa vipengele vya fani huimarisha hali ya mawasiliano ya tungo. Ingawa wasanii hufuata taratibu fulani katika matumizi yao ya lugha, wakati mwingine huzikiuka kwa sababu maalum, kama vile kuwapa wahusika nafasi moja kwa moja kuongea ili tujue ugugumizi wao, ububu, ulevi, ugonjwa au tuone hali ya lugha iliyo katika udhibiti wao, ambayo yaweza kuwa Kiswahili safi, sanifu, au sheng.

Ingawa watunzi wa fasihi wana uhuru katika matumizi ya lugha, watunzi wa nyimbo na ushairi wana uhuru zaidi. Sio tu katika kuchezea mpangilio wa vipashio vya maneno bali pia mpangilio mzima wa fungu la maneno au hata mpangilio mzima wa mishororo na hata beti. Uhuru huu katika sintaksia na mofolojia huendelezwa kwa namna ambayo haitatizi fonolojia na uibukaji wa maana katika tungo.

Swala la lugha limepatiwa uzito mkubwa kwa sababu ya ule uwezo wake wa kuwasilisha mawazo kinyume na vile vipengele vya fani, ambavyo havina uwezo wa kujieleza kama ambavyo lugha hutumiwa kufafanulia maswala, yanayoihusu. Lugha ya nyimbo au ushairi sawa na lugha ya sanaa zote kwa jumla ni lugha bunifu, husishi na inayotekeleza jukumu la kuwasilisha ujumbe. Kwa sababu hii mwimbaji yeyote apaswa kutambua kwamba jukumu la kazi yake ni kuwasilisha.

Kwa sababu hiyo yampasa kila mtunzi kuhakikisha kwamba hata iwe ni kidhahania, ana picha halisi ya hadhira anayoilenga. Hivyo ala zake za muziki zapaswa kuzaa mazao bora na ambayo yapaswa kuwafikia waliokusudiwa kwa uwazi na unyoofu. Matumizi mabaya ya lugha humtenga msanii na hadhira yake au mawazo .

Lugha yoyote hujengwa na maneno ya maumbo mbalimbali na mpangilio mzuri wa maneno hayo huleta maana iliyokusudiwa. Hata hivyo, si jambo la lazima katika nyimbo, kwani mpangilio wa maneno si lazima uitikie kanuni za kisarufi.

Kulingana na Matheru, (1981:76) lugha ni kitu badilifu, elezevu na funizi. Udhaifu wake umo katika kukosa uwazi na udhihiri katika maana na hali linganishi kubadilika kwake na kutodumu

kwake, ugumu na ukosefu wa uelekevu na hali ya kukaidi baadhi ya mambo. Lakini katika nyimbo (kama ilivyo katika sanaa zingine) ule udhaifu wa lugha humpa msanii mvuto katika uteuzi wa namna ya kuwasilisha. Nyimbo (ushairi) haipaswi kubanwa kwenye kiwango cha lugha asilia na lugha sanifu. Ingawa yaweza badilisha kiwango chake ikitegemea mada na matumizi ya msamiati ya viwango mbalimbali vya maana.

3.1.2.1.2 Uteuzi wa msamiati

Hapa tunaangalia kama msanii ameteua msamiati vizuri au vibaya. Msanii ana uhuru wa kutumia msamiati, lakini anapaswa kutathmini uwezo wa msamiati wake kisha kuitolea hadhira yake maelezo. Kuhusu maana (ikiwa ni ngumu). Maneno hutumika vizuri kwa njia asilia yakiteuliwa kwa makini.

Hali ya uteuzi wa neno muafaka huzingatiwa sana katika nyimbo. Neno muafaka huwa tu muafaka katika matini au muktadha fulani – ndiyo maana ufaafu wa fungu hauwezi kutegemea tu neno moja. Msanii huitumia lugha kuipuka ule udhaifu wake asilia kwa kutumia malighafi inayofaa. Hufanya hivyo kwa kutumia maneno yaliyo ya kawaida kwa njia maalum. Hii humwezesha kujieleza kwa ufasaha katika maneno aliyoyachagua. Kila neno huwa huria kiasi kwamba laweza kutumika kwa njia nyingi, na kuzua maana nyingi. Nyimbo hupata nguvu kwa kutumia maneno ya kawaida. Kile ambacho huipa nguvu ni uteuzi mzuri, mpangilio mzuri, uhusiano mwema na mazingira, wahusika, na mikatiko ya matukio katika nyakati faafu. Mbinu nzuri za kupangilia maneno hayo hutupa mazao yenye kugusa hisia na kuathiri fikira zetu.

3.1.2.2 Mandhari/mahali

Mandhari katika kazi ya fasihi ni mahali ambapo tukio linatendeka, Cuddon (1979: 620) anafafanua mandhari kuwa ni wapi na lini katika tamthiliya au shairi. Kwa maneno mengine Cuddon anataka kusema kuwa mandhari ni mahali katika mazingira ya wakati fulani ambapo mahali na wakati husaidia kubainisha muktadha. Wamitila (2008; 351) anasema kuwa mandhari hurejelea wakati na mazingira ya kijiografia ambayo yanakuwa msingi muhimu katika kazi ya kafasihi. Mandhari huweza kuwa nguzo muhimu ya uhusika; pale ambapo matendo ya wahusika yanafungamana na hata kufumatishwa na mazingira wanamojikuta. Mandhari huweza kufungamana kwa kiasi kikubwa na maudhui na dhamira zinazopatikana katika kazi inazohusika. Kuna aina mbali mbali za kuainisha mandhari.

3.1.2.2.1 Mandhari halisi

Waimbaji wengi hutumia mandhari halisi, inayoonekana na inayofikika. Mandhari ya kijiografia ni nguzo muhimu katika nyimbo. Kanuni ya ushabihiki kweli inasisitiza uhusiano wa karibu kati ya ulimwengu wa kibunifu na ulimwengu halisi kwa kumfanya msikilizaji aweze kuamini kuwa matukio, mazingira na maingiliano ya wahusika yanatokea katika ulimwengu huo wa kibunifu.

3.1.2.2.2 Mandhari ya kidhahania

Katika usawiri wa mandhari sifa hii inajitokeza zaidi katika kazi za kifasihi ambazo zinakiuka matarjio ya kila “ukawaida” Uliozoeleka, mambo ambayo yanakiuka uhalisi huo na kuingia ulimwengu usiokuwa wa kawaida. Nyimbo nyingi anazoiimba Anastacia Mukabwa zimezingatia mandhari ya kidhahania.


3.1.2.2.3 Mandhari ya kiishara

Mandhari huweza kutumiwa kwa namna ambayo inafanya kuwa aina fulani ya ishara. Matumizi ya ishara katika fasihi hayafungwi tu kwenye matumizi ya lugha au mbinu za kimtindo. Mandhari huweza kuwa nyenzo nzuri na muhimu ya ishara. Mfano mzuri wa aina hii ya mandhari inapatikana katika wimbo “*Manamba wa matatu*’ ambapo tutajadili katika sura ifuatayo.

3.1.2.3 Umbo na mtindo

Dhana hizi ni za kimsingi katika uchanganuzi wa fani. Umbo ni dhana pana ya kijumla. Katika fasihi tuna umbo la nje kama vile ‘sura’ ‘beti’ na sura ya ndani ‘kama vile jazanda’. Mtindo ni elementi muhimu sana katika fasihi. Ili kuweza kubainisha sifa za kimtindo katika nyimbo, mchanganuzi anapaswa kuchunguza mambo kama vile uteuzi wa msamiati, wa mwimbaji, miundo na mipangilio ya sentensi, uteuzi wa matumizi ya tamathali za usemi, jazanda na kadhalika.

Ni dhahiri kwamba neno ‘umbo’ ni pana na hujumuisha fani, mtindo na Muundo.



3.1.2.4 Ishara

Kwa mujibu wa Madumula (2009:131), neno “ishara’ kama istilahi ya kifasihi ni lile lililo sawa na neno la kiingereza la “symbol’. Na neno hilo la kiingereza linatokana na neno la *kiyunani* ‘*symballein*’ ambalo ni kitenzi chenye maana ya ‘tupia pamoja’ nomino yake ni ‘symbolon’. kwa maana ya ‘alama’ ‘nembo’ au dalili/ishara. Ni kitu hai au kisicho hai ambacho huwakilisha kitu kingine.

Zipo ishara za aina mbalimbali, kwa mfano zipo ishara za jadi (kutokana na kukumbana nazo katika usomaji wa mashairi au nyimbo) inakuwa rahisi kuzielewa na kuona jinsi zifanyavyo kazi. Kwa mfano, ishara za mauti au kifo au ukosefu wa matumaini-‘bundi’ ‘kuchwa kwa jua; ishara za matumaini au maisha mazuri – sauti za ndege, ‘mimea’, asubuhi, ‘maua’ ‘maji’ ‘mvua’. Kwa mfano, watu husema kuwa dalili ya mvua ni mawingu yaani watu waonapo mawingu huona mvua ndani yake kiasi kwamba watu hawashtuki wala kujiuliza mvua inapoanza kunyesha kwani waliona ishara. Kitu kitarajiwacho kilijificha katika hali fulani tunayoiita ishara au dalili.

Ishara zimekumbwa katika maisha ya mwanadamu na hivyo kuwa kitovu katika tamaduni mbalimbali. Hakuna utamaduni usio na ishara zake. Hata hivyo, katika fasihi inawezekana kabisa msanii akatumia vitu fulani kwa kusimamia ishara zake mwenyewe kwa makusudi yake maalum. Anastacia Mukabwa ametumia “*kiatu*” kama ishara katika albamu yake ambayo tuli jadilia katika sura ifuatayo.

3.1.2.5 Toni

Uchanganuzi wa nyimbo hauwezi kuepokana na suala la sauti ya mwimbaji. vile anavyoimba mbele ya hadhira, na anavyoonekana. Toni inaweza kuangaliwa kwa namna mbili.

Kwanza, kama dhana dhahania ya kisauti inayohusishwa na utungo ambayo hufumbatwa na utungo huo. Wahakiki huielezea toni kwa kutumia maneno au maelezo kama; toni ya ucheshi, toni ya mzaha, toni dhati, toni kali, toni ya uchungu na toni ya huzuni. Pili kurejelea usikiaji wa sauti ya nyimbo. Usikikaji huu unaweza kuathiri ujumbe au maana katika utungo wa nyimbo zinazohusika kwa kuusisitiza au hata kwenda kinyume nao. Ni rahisi kuipata toni ya maneno

yanayosemwa lakini kwenye utungo wa nyimbo inamlazimu msomaji kuelewa muktadha, na uteuzi wa msamiati.

Toni, kwa maelezo ya Msokile, . (1993: 93) ni tokeo la uhusiano wa mwandishi na kazi yake au hadhira yake. Anasema kwa kawaida, wahakiki hutumia istilahi “msimamo” kurejelea uhusiano wa mwandishi na kazi yake au kwa hadhira yake au vyote. Msimamo hii kama inavyoonekana katika kazi yenyewe, huvyaza au hufinyanga toni. Msomaji hudhihirisha toni, kupitia mabadiliko ya sauti na hali, lakini mtunzi lazima ategemea ala zake za usemi katika mamlaka yake au udhibiti wake.

Naye Murray (1978:163), anasema kuwa, toni ni usemi wa msemi wa kifasihi kwa, msikilizaji au uhusiano wake kwa msikilizaji au kazi. Kwa hivyo msimamo na uhusiano wa toni hutupa msimamo wa mwandishi na uhusiano wake kwa hadhira na kazi ndivyo huzalisha toni. Toni ni muhimu sana katika kupimia matokeo ya kazi na ishara zinazotokea kwa sababu ya ule mguso wa hisia, athari zake na aina ya taswira zinazojengeka.

3.1.2.6 Wahusika/uhusika

Jonathan Culler katika kitabu chake cha structural *poetics* (1945:35) anasema kuwa uhusika ni kipengele cha msingi katika fasihi simulizi, kwani kila tukio lipo ili kumfafanua mhusika na maendeleo yake. Naye Barthes katika kitabu hicho hicho anasema kuwa mhusika ni kitu kilichochoywa kwa fikra (maneno) kwa msingi wa vielelezo vya kitamaduni, kwa maana kwamba mhusika wa fasihi ya jamii fulani ataeleweka vizuri na kwa urahisi zaidi na jamii hiyo husika. Wahusika katika nyimbo hutazamiwa katika njia zifuatazo.

- a) Kama mtu binafsi kwa sababu ni zao la upekee usioweza kujirudia.
- b) Kama mtu tabaka kwa sababu ni kiwakilishi cha kijamii kinachosimamia tabaka au kikundi maalum na maendeleo maalum ya kipindi maalum cha kihistoria.
- c) kama mtu jamii kwa sababu ni mtu mwenye sifa za mtu na za kijamii. Kutokana na ufafanuzi huu wa uhusika, tunaona wahusika ni watu au viumbe katika kazi ya fasihi waliokusudiwa kuwakilisha tabia za watu katika maisha halisi. Anastacia Mukabwa amezingatia aina hizi mbili za wahusika katika albamu yake.

3.1.2.7 Tamathali za usemi

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001:77), tamathali za usemi ni ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno ili kuleta maana mpya au msisitizo. Kwa hivyo tamathali za usemi ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine.

Naye Msokile (1992:72) anasema kuwa tamathali za usemi ni maana au nahau au usemi ambao hutumiwa na waandishi wa fasihi ili kutia nguvu na msisitizo katika maana, mtindo na pengine sauti katika maandishi hayo. Msokile anashadidia kuwa tamathali za usemi hutumiwa kuipamba kazi ya sanaa ya kifasihi kwa kuongeza utamu wa lugha. Ifuatayo ni mifano ya tamathali za semi.

3.1.2.7.1. Sitiari

Encyclopedia Americana (1997:1996) juzuu la pili inaeleza tamathali ya sitiari kwamba ni ulinganisho kati ya vitu viwili tofauti hivi kwamba kimoja kinapewa sifa za kingine. Sitiari hukuza sifa ya ulinganisho kwa kusema kitu fulani ni kingine. Tamathali hii ni muhimu katika

kujenga taswira. Kwa mujibu wa Wamitila (2011:202) sitiari ni tamathali ya usemi ielezayo sifa za kitu fulani kwa kusema kuwa ni kingine. Kwa hali hii tunaweza kusema kuwa sitiari imejengeka katika uhamishi wa maana. Aidha Wamitila anaeleza kuwa matumizi ya sitiari hulenga hisia au fahiwa fulani au kujenga picha au taswira fulani. Kinachodhihirika hapa ni kuwa sitiari zinahusu uhamishi wa maana na uhamishi huu huchangia maana ya kazi hasa katika fasihi. Matumizi ya sitiari yamefungamana na matumizi ya jazanda ambazo hutumia picha kuelezea hali au kitu na hukuzwa kutokana na maelezo au tamathali za usemi kama kukuza na kujenga maudhui katika nyimbo.

3.1.2.8.1 Aina za sitiari

Tunaainisha sitiari zifuatazo;

(a) Sitiari hai/tendi

Hii ni aina ya sitiari ambayo huhitaji ubunifu mkubwa ili kueleweka. Msomaji au msikilizaji huweza tu kuelewa vyema ikiwa pana maelezo ya ziada ya kimuktadha ambayo yatamsaidia kutatua utata unaosababishwa na kilinganishi ambacho si cha kawaida. Sitiari za aina hii zinapatikana sana katika ushairi na nyimbo ambazo zina ubunifu mkubwa wa matumizi ya lugha. Mchambuzi yeyote anayekabiliana na maneno ambayo hayamo katika maana au ruwaza za kimaana za kila siku, analazimika kuwaza sana.

(b) Sitiari fiche

Sitiari ambapo kilinganishi hakitajwi waziwazi bali sehemu yake ndiyo inayodokezwa na ilikuweza kuweza kuzielewa sitiari za aina hii hutegemea uwezo wa kuhusisha vitu au sehemu zinazotajwa ili kuweza kutambua msingi wa sitiari inayohusika.

(c) Sitiari dhana

Hii ni sitiari ambayo hutokea pale ambapo kitu fulani au kitu kilichoko katika mwanda fulani maalum kinaeleweka kwa kukiweka katika muktadha au mwanda mwingine tofauti. Katika sitiari ya kidhana, tunakielewa kitu fulani kwa msingi wa kitu kingine.

(d) Sitiari pana/mzizi

Hii ni sitiari ambayo imefungamanishwa na lugha kiasi kwamba watu au wazungumzaji na watumiaji wa lugha hawaiangalii tena kama sitiari. Kwa mfano, watu mara nyingi hutumia “mlima” “ndovu” kama sitiari ya ugumu au matatizo. Sitiari za aina hii hutofautiana kutegemea tamaduni zinazohusika. Anastacia Mukabwa ametumia *kiatu* kudhibitisha kauli hii kwamba kiatu ni hali ngumu ya maisha

3.1.2.7.2 Chuku

Mbtaiah. (2001:6) anasema kwamba chuku ni tamathali ya usemi inayotumia lugha ya kutilia chumvi, aghalabu kwa madhumuni ya kusisitiza jambo au hali kukuzwa kupita kiasi. Aidha mbinu ya chuku hutumiwa kupunguza sifa za kitu au mtu kwa lengo la kumdunisha. Nia ya kutumia chuku ni kulifanya jambo fulani litokezee kwa uwazi zaidi, kuikuza sifa fulani au kumfikirisha msomaji kwa kuona uzito uliopo. Kwa msingi huu huwa pana ukinzani kati ya hali inayosemwa na ukweli wenyewe. Hii ni sifa ambayo inahusishwa kwa kiasi kikubwa na kinaya, kwa mfano ni rahisi kwa ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko kwa tajiri kuingia Ufalme wa mbinguni; hili ni chuku maarufu ya Bibilia. Kinachosisitizwa na ugumu wenyewe ni kuwa ni vigumu sana kwa tajiri kuingia Ufalme wa Mungu kwa kuwa kinachomshughulisha tajiri sana ni mali yake. Hii hata hivyo haina maana kwa vile ngamia hawezi. Kwa msingi huu basi pana ukinzani fulani. Ni bayana kwamba chuku imetumika katika wimbo *manamba wa matatu* kutilia mkazo tabia za watu wasiokuwa na msimamo.

3.1.2.7.3 Tasifida

Wamitila K. (2003: 194) anafafanua kuwa tasfida ni matumizi ya maneno ya kupunguza ukali au uzito fulani, badala ya mhusika kutumia lugha inayoficha makali hayo. Aghalabu tasfida hutumiwa baina ya watu ambao hawana budi kuwekeana heshima katika mazungumzo yao. Mbinu hii ya kazi ya kifasihi hutumiwa kwa maongezi ya kila siku. Kuficha ubaya au uovu fulani kwa kutumia maneno au lugha ambayo inapunguza makali ya uozo, ubaya au uovu unaozungumziwa. Anastacia Mukabwa ametumia tasfida kupunguza ukali kwa kutotaja watu moja kwa moja, hivyo basi ametumia maneno kama kiatu, manamba, Farao kurejelea watu bila kuwataja kwa majina.

3.1.2.7.4 Tashihisi

Ni tamadhali ya usemi ambapo kitu kisichokuwa na uhai kinapewa sifa za binadamu na kuonekana kutenda kama binadamu kwa mfano usiku ulipoanza kuukumbatia ulimwengu kwa mahaba mazito wangwana walianza kuwasili Koinange kwa magari mazito tayari kukata kiu ya maumbile. Kilicho wazi katika mfano huu ni kuwa usiku hauna mikono ya kuukumbatia ulimwengu –hauna uhai bali mwandishi ameupa sifa ya binadamu ya kuweza kukumbatia. Tamathali hii imetumiwa na Anastacia kwingi katika nyimbo zake ili kuleta mvuto wa kisanaa na athari fulani ya kihisia.

3.1.2.7.5 Tashbihi

Senkoro, (1982:14) anasema katika tamathali hii watu ama vitu viwili au zaidi hulinganishwa na watu ama vitu vingine kwa kutumia maneno kama, mithili, kama, kwamba, mfano wa, na mengine ya aina hiyo “Huu ni mtindo wa uneni wa kifani ambao kwao kitu kimoja au zaidi hulinganishwa au hufananishwa na kitu au vitu vingine tofauti vilivyo na ufanano au ushabihiano

fulani wa hali ya utendaji au maumbile, mathalani, sura, rangi, na jinsi ya kujimudu. Kwa kawaida tashbiha huonyeshwa kwa kutumia maneno kama, mfano wa, mithili ya, vile, ja, sawa sawa na maneno mengine yenye kuonyesha mlinganisho kati ya vitu mbalimbali.

Msokile M. (1992:54) anafafanua kuwa aina hii ya tamathali hutumia mlinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viuganishi. “kama’ mfano, wa’ ‘mithili ya’ ‘sawa na’ na’ mfano wa’.

Mwandishi hutumia ulinganishi huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini kwa mfano Anastacia Mukabwa ametumia tashbihi katika wimbo: Usiwe! Usiwe! *Kama manamba wa matatu* anayesema twende kasha anabaki nyuma.

3.1.2.7.6 Dhihaka

Kwa mujibu wa senkoro, (1982:20) Hii ni aina ya kejele. Ni tamathali ambayo ina ubezi muali, jahili unapopenya kweli. Hii pia hutumia mbinu ya kutoa maneno ambayo kijuujuu yanasikika vizuri sana masikioni wakati ambapo huwa yamekusudiwa yatoe maana iliyo kinyume chake kabisa. Msokile (1993:79). Anaeleza kama, ”maelezo au masimulizi yaliyokusudiwa kubeba jambo kisirisiri. Ni maelezo yanayomdunisha mtu kisirisiri”

Kuhusu tamathali hii, Wamitila[2003:94] Anasema kuwa msemaji au mwandishi hutumia usemi unaoficha hisia zake kumhusu mtu au kuihusu hali fulani. Kimsingi pana kinaya fulani katika maneno yaliyotumika. Sababu kuu ya kutumia dhihaka ni kumcheka mtu au kumkera mtu Anastacia Mukabwa ametumia dhihaka kukejele watu katika jamii walio na tabia ambayo ni kinyume na maadili katika wimbo *Kiatu kivue* na *Manamba wa matatu*.

3.1.2.14 Takriri

Takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi ya sanaa kama anavyosema Msokile M.(1992:61). Lengo kuu la mwandishi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo ni kutilia mkazo jambo linaloelezwa. Mbina hii imetumika kwa uwazi katika nyimbo za Annastacia Mukabwa kama kiitikio.

3.1.2.7.8 Mdokezo

Hii ni mbinu ambapo mwandishi anaukatiza usemi fulani na kumwachia msomaji kumaliza. Aghalabu huwa pana vielekezi vinavyoweza kumsaidia msomaji katika kukamilisha usemi huo. Mdokezo unaweza kutumiwa kuashiria maarifa fulani. Inawezekana pia ukasababishwa na sababu ya tasifida. Mwimbaji Anastacia Mukabwa ametumia mbinu hii kiasi kwamba imejitokeza dhahiri katika mtindo wake.

3.1.2.8 Hitimisho

Kuna baadhi ya mbinu na matumizi ya lugha kama taharuki, mjadala nafsia, mbinu rejeshi na zinginezo ambazo hazingii katika uhakiki wetu wa fani katika muktadha wa nyimbo, kwa hivyo hatukujadili.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA FANI KATIKA NYIMBO ZA ANASTACIA MUKABWA

4.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tulieleza mambo ya kimsingi kuhusiana na utafiti huu. Mambo hayo yamekuwa nyenzo ya kutuongoza katika utafiti wetu. Tutaelezea misingi ya kinadharia ya uhakiki wa mtindo katika kila mojawapo ya fani na kuitolea mifano ya kijumla, kila inapobidi ili kuweka wazi maelezo yetu. Kwa kuzingatia mwelekeo huu mpya wa uhakiki wa kimtindo tulitumia vipengele vinne vya kihakiki ambavyo ni:

Lugha ya kitamathali na mtindo, uteuzi na mtindo, uchimuji na mtindo, muwala na mshikamano na mtindo.

a) Lugha ya kitamathali na mtindo

Kiwango hiki tumechunguza matumizi ya tamathali za usemi zilizotumiwa na msanii Anastacia Mukabwa katika nyimbo tofauti. Mojawapo wa tamathali hizi ni sitiari ambayo imetumika sana katika baadhi ya nyimbo. Kwa mfano, wimbo *kiatu kivue* ambao tumejadili.

b) Uteuzi na mtindo

Anastacia Mukabwa amezingatia sana suala la uteuzi wa msamiati ambao upo kwenye sajili ya kidini. Uteuzi wake wa msamiati umeongozwa na kaida za utunzi wa nyimbo na matini husika. Ametumia msamiati wa kawaida ambao ni rahisi kuelewa lakini ameutumia kwa makini kuwasilisha ujumbe na maudhui.

c) Uchimuji na mtindo

Uchimuji huu umetokea katika kiwango cha kisintaksia na kisemantiki ambapo tutapata kuona ufasaha na wepesi wa mtiririko katika nyimbo. Mazingira na matumizi ya maneno yametumiwa kwa njia mwafaka.

d) Muwala, mshikamano na mtindo

Kiwango hiki kitachunguza vipengele vya kifani ambavyo huleta mshikamano wa kazi yoyote ya kifasihi. Yaani tumezingatia mjumuiko wa vipengele vya kisanaa ambavyo huwasilishwa na umbuji ulio na upekee kwa mtunzi maalum.

Kulingana na Wamitila (2008:521)maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi. Maudhui hujumulisha dhamira, itikadi, msimamo, maadili, mafuzo na falsafa, kwa hivyo maudhui yaliyomo katika nyimbo hayawezi kumfikia msikilizaji bila kuwepo na nyenzo za kupitisha au kuwasilisha.Uhusiano uliopo kati ya fani na maudhui ni wa kutegemeana. Hivyo basi maudhui yatajitokeza tutakapojadili vipengele vya fani katika nyimbo.

4.1 Lugha

4.1.1 Uteuzi wa msamiati

Kimsingi, linalozingatiwa ni kwamba uteuzi mbaya wa msamiati utavunja mioyo ya wasomaji na kuvunja mawasiliano pia,ambapo iledaraja la kuwavusha watu kimaana litakuwa limebomolewa. Kazi za sanaa husifika kwa sababu ya ule ufundi wa kuwasilisha ufundi huu kimsingi unategemea namna msanii anavyochagua maneno yake kutoka hazina kubwa ya malighafi ya leksia. Hili linatupa uwezekano kwamba maneno hata sita yanaweza kuwakilisha kitu kimoja kimaana. Katika haya yapo ambayo yatafaa zaidi kwa uzito na msisitizo kuliko mengine katika miktadha, matini na mazingira maalum. Kwa sababu hii tunadai kwamba pale ambapo mwimbaji atafanikiwa kuteua neno mwafaka na kulitumia katika mazingira yanayofaa na kulipea msisitizo fulani analolipa uzito fulani katika muktadha fulani atakuwa amefanikiwa.

Kwa mfano: wimbo *manamba* ubeti wa kwanza

*Usiwe! Usiwe! kama manamba wa matatu,
Anayesema twende kiisha anabaki nyuma,
Manamba ni mtu yule jumapili yu kanisani
lakini matendo yake hayapendezi mungu.
Kupiga dala dala yeye anasema twende,
kisha ikiondoka yeye anabaki nyuma*

Kutokana na mfano huu ni dhahiri kwamba msanii ametumia neno *manamba* kisitiari ili kurejelea mtu asiyekuwa na msimamo na mienendo mizuri. Neno *manamba* lina maana ya utingo lakini katika muktadha huu na mazingira haya lina maana ya waumini ambao ni kikwazo kanisani. Katika muktadha wa kijamii watu hawa hulinganishwa na watu wasiopenda maendeleo. Si lazima msamiati uliochaguliwa uwe wa kale, wa wastani, mwepesi au wa Kiswahili tu, ila hata wa lugha zingine madhali wakubali kubadilika kiumbo ili kuoana na mazingira ya lugha pokezi.

Ni kutokana na madai haya tumegundua msanii Anastacia Mukabwa ametumia msamiati mbali mbali katika nyimbo zake. Kwa mfano: *Wimbo heshima*; ubeti wa tano: mshororo wa pili na wa nne:

*Leo wanakuita kikarakosi kesho watakuita bosi
Watakupigia saluti watakusalimia kwa heshima*

Maneno “*bosi*” na “*saluti*” yametoholewa kutoka lugha ya Kiingereza na kubadilishwa kisauti ili kuoana na mazingira ya lugha pokezi. Vile vile wimbo *zinzilela*, ambao una asili ya kizulu lakini umeborongwa kisauti na kuingiliana na lugha ya Kiswahili.

*Wimbo zinzilela (ubeti 1)
Zinzilela wakata na mule zizilela zimilela,
Ee Bwana nakuinua niki kumbuka ulikonitoa
Kwenye maisha ya aibu na kunifanya wa dhamaini x 2
Kama si wewe ningekua wapi kama
Si wewe ningetitwa nani,
Ni ngekuwa, nimekufa kwenya shimo la uharibifu x 2*

Anastacia Mukabwa, kwa kiwango kikubwa amefanya uteuzi wa maneno sio tu yanayofaa na kuoana na mazingira bali pia yanayobeba uzito huku yakichukuana vyema na wakati, ploti mbali na kuleta ile toni inayotarajiwa katika mazingira maalum. Uteuzi alioufanya ni mzuri na unachukuana na mandhari aliyoyashuhudia msanii. Kwa mfano, katika wimbo “*kiatu kivue*” msanii ametumia msamiati wote kwa makini na kuutumia katika mazingira mwafaka.

Wimbo **kiatu kivue** : ubeti 2:

*Hata leo Mungu anena nasi hicho kiatu kivue,
Kiatu ni dhambi uzifanyazo nakwambia kivue
Ukahaba unaoendeleza kando kando ni kiatu kivue.
Wivu na masengenyo yanayokuja ni kiatu kivue.
Kitakupeleka jehenamu hicho kiatu kivue
Kualia wake wa wenyewe kutongoza waume wa
wengine ni kiatu kivue.*

Kutokana na ubeti huo, kuna ushahidi tosha kuwa msanii ametumia msamiati kwa makini na hadhari. Karibu maneno yote ameyateua kwa njia nzuri yanawafiki katika kuhusiana na katika muktadha. Uzito wake watokana na mtindo wa msanii wa kumhusisha msomaji moja kwa moja. Haya yanadhihirika katika mishororo ya pili, na tatu.

*Kiatu ni dhambi uzifanyazo
Ukahaba unaoendeleza ni kiatu*

Mishororo hiyo inabeba maana nzito katika matini pia inachukuana na hadhi ya wahusika lengwa. Ushahidi wa uteuzi mzuri wa msamiati unatokea katika nyimbo *manamba* na ‘*heshima.*’ katika albamu kiatu kivue.

4.1.2 Aina ya msamiati

Mbali na kile kiwango cha uzito, wepesi na uwastani wa msamiati tunaangalia pia viwango vya mofolojia, ukawaida na ukosefu wa ukawaida katika msamiati. Msanii ametumia msamiati mzito na wa kawaida wa asili mbalimbali. Kuna baadhi ya maneno yaliyokopwa kutoka lugha ya Kizulu katika wimbo *zinzilela* maana yake ni “utukufu” vile vile maneno mengine yamekopwa kutoka lugha ya Kiingereza neno “bosi” lina maana ya “Boss” watakupigia “saluti” lina maana ya “Salute” Smaart (waridi) mifano hiyo ya maneno na mengine mengi imetumiwa kwa ufasaha katika mazingira inayofaa. Kuna baadhi ya maneno ambayo uzito hupatikana tu yakitamkwa kwenye asili yake: kwa mfano neno “bosi” likitumiwa na asili ya Kiingereza linakuwa na uzito ukilinganisha na neno “mkuu” au “mkurugenzi” mwajiri” katika lugha ya Kiswahili.

Ushirika wa sintaksia na semantiki una sehemu muhimu hapa katika kuleta ufasaha au wepesi wa mtiririko katika nyimbo. Mazingira ya matumizi ya maneno hutegemea kaida za sintaksia, katika kupata unyofu wa kisemantiki kwa mfano wimbo *manamba* ubeti wa 3.

*Mwendapo kanisani hamwendi kuniabudu,
Mwaenda mjulikane muone jamaa wa kanisa,
Tatizo liwapatapo kanisa liwasaidie,
lakini moyoni hamkuweka Mungu wenu,
Badilisha mienendo yenu.
Badilisheni tabia zako ili nitakaporudi
Niende nanyi milele mbinguni.*

Tunapoangalia ubeti huu, uwasilishaji ni wa moja kwa moja ambapo mpangilio wa maneno na msamiati unachukuana kimitiririko.

Mfano mwingine ni wimbo: *kiatu kivue ubeti* (1)

*Mungu alinena na Musa hicho kiatu kivue x 2
Ulichotoka nacho kwa Farao nakwambia kivue
Mahali hapa ni patakatifu hicho kiatu kivue.*

Katika wimbo huu *kiatu kivue* neno kiatu lina uzito ambao unatokana zaidi na matumizi ya msamiati “kiatu” kitamathali na kwa kufumba. “Kiatu” ni neno lepesi na la kawaida ambalo hurejelea kifaa kinachovaliwa mguuni Lakini limetumiwa kwa njia tofauti kulingana na mazingira na jinsi ambavyo limetumiwa kijazanda, kwa njia hiyo matumizi haya yana uzito fulani kisemantiki. Tunapotaja ufasaha wa msamiati, neno ufasaha hujumuisha mambo mengi, nayo ni pamoja na asili ya neno, matini iliyotumika, nguzo za maana linayowakilisha, mpigo, uongovu na usitiri wa maana katika mawasiliano, uwezo wake wa kuweza kuathiri msimamo wa msomaji, ufaaji wake katika muktadha, uhusiano mzuri na maneno mengine, uwezo wake wa kuhamisha sifa hasa za kimaana, uwezekano wa kuweza kutumia katika miktadha mingi na pia uwezo wake wa kuwakilisha maana nyingi na pana.

Mfano wimbo: manamba: ubeti 1

*Usiwe! Usiwe! kama manamba wa matatu
anayesema twende kisha anabaki nyuma.*

*Manamba ni mtu yule jumapili yu kanisani
lakini matendo yake hayampendezi Mungu.
Kupiga daladala yeye anasema twende
kisha ikiondoka yeye anabaki nyuma.*

Wepesi wa msamiati alioutumia msanii katika wimbo huu *manamba* hauna athari kubwa kwa msomaji na umezoeleka sana na matumizi yake ambayo yamewasilishwa kwa urahisi bila vizuizi. Wengi huona msamiati wa aina hiyo kama umechakaa na ambao hutumika katika mazingira ya kawaida yaliyozoeleka sana lakini ni vigumu kupata ujumbe uliopo. Yafaa

kusomwa kwa makini ili upate kuelewa mazingira na muktadha uliotumiwa ndiposa upate ujumbe.

Katika kuhakiki aina ya msamiati uliotumiwa katika nyimbo hizi tumeangalia uanishi wake katika makundi ya nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, viunganishi, vimilikishi, vionyeshi na kadhalika. Kwa kuhakiki mifano miwili ya sentensi tumegundua kwamba kila mojawapo wa leksia zake huwa na uamili mkubwa sana katika sanaa. Katika usemi wa kawaida watu hulenga tu kuwasiliana. Lakini katika fasihi hulenga kuwasilisha kwa mvuto. Hapa wasanii hujali sana wanavyowasilisha, kwa hivyo, nafasi kubwa ipo ya vivumishi,vielezi,vimilikishi, na viunganishi. Mifano ifuatayo imetusaidia kuangazia swala hili.

Wimbo: *Heshima*: Kiitikio

Nasema watakusalimia kwa heshima

Kitenzi Kitenzi Kielekezi Kielezi

Kisaidizi kikuu Kihusishi

Wakati wangu wa kubarikiwa ukifika

Kivumishi kivumishi A-ungnifu kitenzi kitenzi

Cha wakati kimilikishi

Watakusalima kwa heshima

Kitenzi kihusishi kielezi

Kutokana na mifano hiyo twaona jinsi kila kundi la maneno yaliyo na uamili wa kuwasilisha ujumbe kufuatana na mpangilio unaofaa. Vielezi na vivumishi vikitumiwa vizuri husaidia kupamba ujumbe kisanii. Hii inafungamana na ufundi mkubwa wa msanii. Kutokana na mifano hiyo, ni thibitisho kwamba kuna mpangilio mzuri sana wa kisintaksia ambapo kila neno limeingia mahali pake. Hatuoni neno lolote lililotumiwa kimakosa maneno yanafuatana kwa utaratibu usiovunja muwala na mifano hiyo inatuthibitishia kuwa utaratibu na mpangilio wa maneno katika tungo za nyimbo ni mzuri.

4.2 Toni

Ni wazi kuwa katika nyimbo hizi kuna aina nyingi za toni ambazo kimsingi zategemea aina ya mawazo anayoyawasilisha msanii na namna alivyowasilisha. Mifano imetolewa kuthibitisha kuwa toni fulani imetumiwa na imetumiwaje. Aina ya kwanza ya toni tunayoiona ni ile inayotokana na sifa za kuisimua, kuajabisha na kushangaza, katika baadhi ya wahusika wanaohusishwa na matukio fulani. Toni ya msisimko inapatikana katika nyimbo *kiatu kivue*, *utukuzwe* na *manamba*. Katika wimbo *kiatu kivue* tunaona sifa za kuisimua. Kiatu kimepewa sifa za ubinadamu na kulinganishwa na tabia za watu ambao wana tabia mbaya vile vile wimbo *utukuzwe* tunapata sifa ya kuajabisha na kushangaza, pale ambapo wanyama wanazungumziwa na kuamrisha waimbe.

Ubeti 2:

*Haya fisi na viumbe mito naipige makofi,
Ndege na waseme amina kubwa wanyama wamuinua
Sifu yaya haya fisi wanabidii mwewe mito na ipige makofi.,
Ndege na waseme amina baba, wanyama wanamuinua sifu
bwana watawala bwana.*

Hali ya kutojali ambayo inadhihirika katika baadhi ya nyimbo kama *Heshima na*

Manamba inatupa toni ya kutojali ambapo kabisa watu hawajali wenzao. Hali hii huleta maudhui ya mahusiano mabaya kama inavyobainika katika mfano huu.

Wimbo *Manamba* ubeti 4

*Enyi watumishi wangu mwasema
mmeokoka na huku kando kando mwakata kondoo mkia
Tabia hiyo itawapeleka motoni nyinyi
Ni kama manamba wanaobaki nyuma,
Badilisheni mienendo yenu, badilisha tabia
zenu ili zitakaporudi niende nanyi milele.*

Toni ya huruma, huzuni kwa wahusika wanaopokea matendo maovu na ya kikatili kutoka kwa wenzao inajitokeza. Twaona jinsi watu wanabaguliwa kwa sababu ya hali yao ya umasikini katika jamii. Kuna hisia zinazochipuza huzuni na toni ya uchungu, hali inayotokana na matumizi ya msamiati uliotumiwa.

Mwimbaji hakuepuka jukumu la kuishauri hadhira yake kwa kuipa mawaidha mbali mbali ya kijamii, kama inavyojitokeza katika wimbo *kiatu* katika *kivue*. Matendo maovu ya kubomoa chochote kizima katika jamii na mahusiano ya kijamii kwa kuchochea ndoa ili kuvuruga uhusiano mzuri familia zetu. Hali ambayo inatupatia toni ya ubomovu.

Mfano ufuatao unadhihirisha hali hii;

Wimbo *kiatu kivue*

Ubeti 2:

*Hata leo Mungu anena nasi hicho kiatu kivue,
Kiatu ni dhambi uzifanyazo ni nakwambia kivue
Wivu na masengenyo yanayokuja ni kiatu kivue.
Kitakupeleka jehanamu hicho kiatu kivue,
Usinzi unaoeneza wewe ni kiatu kivue
Kualia wake wa wenyewe ni kiatu kivue
Kutongoza waume wa wengine ni kiatu kivue
Kitakupeleka jehenamu hicho kiatu kivue
mama hicho kiatu, baba hicho kiatu kivue.*

Msisitizo wa mapenzi ya dhati watokea pia katika ubeti huu. Mtunzi anashauri mshikamano wa dhati katika mahaba hali ambayo inatupa toni ya mapenzi. Kwa ufupi, msanii amezitumia kunga zake za fani vizuri kwa njia ambayo inatuwezesha kupata toni za nyimbo zake tofauti katika utafiti huu. Mwimbaji ameziangalia vyema toni ambazo zatokea wazi katika mazingira aliyoyataka kwa namna ambayo inagusa hisia za wasomaji moja kwa moja na kuathiri upokeaji wao wa mawazo yake. Huu ni ufanisi mkubwa katika fasihi simulizi.

4.3 Mandhari

Mtunzi ametuambia mandhari mbalimbali kwa njia ya kumwezesha kuwasilisha mawazo anayotaka ambayo yanaoana na wakati .Kwa mfano , kuna mandhari halisi ambayo ni nguzo muhimu katika nyimbo, kwa sababu inasisitiza uhusiano wa karibu kati ya ulimwengu wa kiubunifu na ulimwengu halisi. Mandhari mbalimbali ya kijamii yanayojitokeza ni kama vile mapenzi, maombolezo, ulezi mahusiano, uabudu (dini). Mandhari yote yamesawiriwa kwa njia inayodhirihiwa kwa uwazi .Kwa mfano, katika mandhari ya mahusiano tunaona vile watu walivyo wakatili, waovu, fisadi na wenye husuda. Katika wimbo, **Heshima**, wahusika wa aina hii na majukumu yao yanadhihirika vizuri kwa njia inayomfanya msomaji kuyaona kwa uwazi matatizo yanayowasibu watu wenye chuki. Ndio maana msanii anawapa watu tumaini katika ubeti 2.

*Wanaosema hutaolewa watashuhudia ndoa yako
Mara utokapovalishwa pete watapatwa na kigugumizi.*

*Wanaosema wewe ni tasa wataona ukinyonyesha
Mungu aliyemkumbuka Sarah hata wewe utakumbukwa
Nasema watakusalimia kwa heshima x2*

Kuhusu mandhari ya kiishara, kunajitokeza picha au taswira katika wimbo **Kiatu kivue** ni ishara ya mienendo mbovu ya viongozi katika jamii . **Manamba** ni ishara ya watu wasiokuwa na msimamo dhabiti katika jamii, ambapo ishara hizi zimetumika kulinganisha tabia ya binadamu. Badala ya kutaja mtu moja kwa moja mtunzi ameturejesha kwenye ishara.

Kwa hivyo, kila aina ya mandhari imetokea kwa njia nzuri na inayofahamika.Hakutokei mandhari ya kulazimishwa au yanayokinzana na mawazo yaliyotarajiwa kuendelezwa.

4.4 Wahusika / uhusika

Msanii ametusawiria wahusika mbalimbali ambao ni pamoja na Mungu ,wanadamu, wanyama, vitu na hata mahali.Wote wanatokana na utaratibu unaomwezesha msomaji kuona namna walivyotumiwa ingawa hatukuwapitia wote kwa undani tumeangalia baadhi yao.

Vifungu vifuatavyo vilituongoza katika kuona jinsi Mungu alivyosawiriwa.

Wimbo *Heshima* ubeti wa nne

*Mungu wangu wewe ni kimbilio langu
Msaada wangu tena ni tegemeo langu,
Bwana ninakulilia usikie kilio changu.
Farao ni yule shetani anayetesa watoto
Kuwa Mungu ni Ebeneza hata sasa yupo,
msaada watu wa karibu*

Mifano hiyo yatuelekeza kwenye baadhi ya sifa za Mungu katika sifa nyingi alizo nazo. Yeye ndiye Muumba na mtoa vyote viliyomo humu duniani. Kwa hivyo, miliki yote hiyo aliyotupa kutuendeshea maisha yatupasa kutufanya kumwona kama mfadhili mwema ambaye yafaa tujenge uhusiano mzuri naye. Mungu anatuhimiza kutubu kwani yeye ni mwingi katika kutoa toba. Kwa hivyo msanii amemsawiri Mungu vizuri na kumhusisha na sifa na matendo yake.

Kuhusu wahusika binadamu kuna msanii mwenyewe, wasomaji, watumizi wa lugha na wahusika maalum.Hao wote amewachora kwa namna inayowapa nafasi tukawaona pamoja na ule umuhimu wao.Katika baadhi ya nyimbo mtunzi mwenyewe amehusika katika kusimulia na kueleza mawazo yake. Katika kufanya hivyo, nafasi ya kwanza na ya tatu zimetumiwa moja kwa moja amewashirikisha wasomaji wake. Kwa mfano;

Wimbo *Heshima*

Ubeti 1

*Wanaokudharau siku moja watakusalima kwa heshima x 4
Mateso yako ni ya muda Mungu akuandialia ushuhuda,
Daudi alikua mchungu kondoo Mungu akamuinua akawa mfalme.
Leo unaitwa omba omba kesho utaitwa mbarikiwa
Licha unatembea kwa miguu kesho utaendesha gari.*

Mfano huo unatuonyesha nafasi ya masimulizi, maelezo na umuhimu wa wahusika (hadhira). Matumizi haya yanatuwezesha kuamini tungo ambazo sasa hatuzioni zipo mbali na maisha halisi kwa uhusika na wasomaji japo hawamjibu moja kwa moja kunatokea ukamilifu unaotufanya kuamini. Kwa mfano, katika mshororo wa tatu, maskini anapewa tumaini kwamba siku moja atakuwa tajiri.

Msanii pia anatuchorea wahusika wenye hulka mbalimbali, kuna wale waovu na wapotovu na wasioshuriwa wakashaurika amewaeleza katika wimbo *Farao*.

“Farao” ni mhusika katili ambaye alikuwa mfalme wa nchi ya Misiri aliyeamuru watoto wavulana wa taifa la Israeli waangamizwe.

Kupitia usimulizi huu mwimbaji amemsimulia mhusika huyu kupitia nafsi ya pili na ya tatu kumtaja kwa majina. Kwingineko ametumia wahusika kama ndege, fisi, mito, wanyama na vitu.

Twaona kwamba wahusika hao wote wanendeleza ujumbe wa aina fulani japo ni wanyama, mimea na ndege wametumiwa kisitiari kumrejelea mhusika binadamu ambaye hafuati maagizo ya Mungu.

4.5 Ishara

Ishara zimekumbwa katika maisha ya mwanadamu na hivyo kuwa kitovu katika tamaduni mbalimbali . Katika fasihi inawezekana msanii akatumia vitu fulani kwa kusimamia ishara zake mwenyewe kwa makusudi yake maalum. Anastacia Mukabwa katika wimbo wake *Kiatu Kivue* ametumia Kiatu kama ishara ya tabia au mienendo mibovu ya binadamu ambayo ni kinyume na maadili mema ya kijamii.

Kwa mfano ukahaba na wivu zimetumika kama ishara kwa kulinganishwa na kiatu ambacho Musa katika Biblia Takatifu aliamuliwa na Mungu akivue. Ufuatao unaakisi ufafanuzi huu;

Ubeti wa kwanza.

*Mungu alinena naye Musa hicho kiatu kivue x2
Ulichotoka nacho kwa Farao nakwambia kivue
Mahali hapa ni patakatifu hicho kiatu kivue*

Zipo ishara za aina nyingi zilizotumika kwenye nyimbo hizi kwa mfano jina “Musa” ni ishara ya mkombozi ilhali, “Farao” ni ishara ya mtu mbaya au kiongozi dhalimu. “Manamba” ni ishara ya mtu asiyekuwa na msimamo. Ni kupitia ishara hizi tunapata maudhui ya ukahaba, wivu na ubinafsi kwenye wimbo *Kiatu kivue*.

4.6 Ploti

Takriban nyimbo zote zilizomo katika albamu hii zimeendelezwa kwa njia ya ploti ya mtiririko au fululizi. Matukio yameelezwa au kusimuliwa kwa namna ambayo ni ya muwala. Matukio yanaingiliana kwa njia nzuri. Mpangilio wa matukio au maelezo watupa dalili za mwanzo, mwili na hitimisho katika kila wimbo. Sehemu hizo tatu zilipendekezwa na Aristotle ambaye alisema kuwa lazima zote ziwepo katika mtindo aliotumia. Ufuatayo ni mfano katika wimbo *kiatu kivue*.

KIATU KIVUE

Anastacia Mukabwa

*Musa hicho kiato kivue x2
Nataka ninene nawe kivue
Nataka nikutumie kivue
Nataka nikuinue kivue
Nataka nikubariki kivue
Watu wangu waangamia taifa langu la Israeli kivue
Watu wangu wanasononeka watu wangu wanateseka kivue
Nataka nikutume wewe ukaokoe taifa langu la Israeli Kivue.*

*Hata leo Mungu anena nasi hicho kiatu kivue
Kiatu ni dhambi uzifanyazo nakwambia kivue.
Ukhaba unaoendeleza kando kando ni kiatu kivue.
Wivu au masengeyo yanayokuja ni kiatu kivue
Kitakupeleka jehenamu hicho kiatu kivue
Uzinzi unaoeneza wewe ni kiatu kivue
Kualia wake wa wenyewe kutongoza waume wa wenyewe
ni kiatu kivue.*

*Nataka ninene nawe maana ninakupenda kivue
Nataka ninene nawe ili nikuokoe kivue
Mimi sitaki uangamie mimi sitaki upotee kivue
Mimi sitaki uangamie maana mimi ninakujali kivue
Mimi Mungu ni wa neema kivue
Mimi Mungu ni wa upendo kivue*

*Ukitaka Mungu akubariki lazima kiatu ukivue
Ukitaka kuinuliwa ni lazima kiatu ukivue
Wivu uliyo nao wewe ni lazima kiatu ukivue
Hutaki kuona wenzako kama wakiinuliwa wewe Kivue*

*Hutaki kumwona mwenzako akiwa amependeza kivue
Hutaki kumwona mwenzako akiwa ako smart kivue
Tabia uliyonayo mama na kwambia kivue
hutaki kuona ndoa ya mwenzako mume na mke wakicheka kivue
Tabia uliyo nayo mama kivue,
nakwambia badilika Kivue,*

*Hutaki kuona huduma ya mwenzako ikisonga kivue
Mbele kivue, hebu kivue
Jamani kivue kiatu cha nyumba ndogo kivue
Kiatu cha ulevi , kiatu cha uzinzi kiatu cha kivue*

*Ooh ooh ooh kivue kiatu kiatu kivue kivue
(Mungu anena nawe hicho kiatu kivue x2)*

*Waliowadhamini waume wa wenyewe iwe mwisho Kivue
Kualia vitumbua mume wa wenzio iwe mwisho kivue
Kupaka wanja kwa mume wa mwenzio iwe mwisho Kivue
Nataka nikupe mumeo nataka kikupe nyumba yako nataka kivue
Nikuinue..... nataka nikuinue mume wako kivue
Niinue nyumba yako kivue,
niinue mke wako nikubariki kivue,
Mchumba kivue kiatu cha nyumba ndogo kivue
Mungu anasema na wewe hicho kiatu kivue
aah aah aah kivue.*

Anastacia Mukabwa anasimulia historia ya Biblia kumhusu mhusika Musa ambaye anaamrisha na Mungu avue viatu katika utangulizi wa wimbo huu. Sehemu ya pili ambayo ni mwili Anastacia anafafanua kinagaga maana ya kiatu katika muktadha wa kijamii; anasema kuwa kiatu ni tabia hasi ya binadamu. Hatimaye anahitimisha wimbo kwa kutoa onyo kwamba watu waachane na dhambi kwani mwishowe wataangamizwa.

Mfano huo unawakilisha sehemu tatu ambazo ni mwanzo, mwili na mwisho. Maneno yamepangwa kwa namna ambayo inaonyesha kuwa sehemu fulani ni mwanzo ,kati na mwisho. Hata hivyo, kuna nyimbo ambazo hazionyeshi moja kwa moja kuwa ni mianzo.

Sehemu ya mwili ambayo ndiyo yenye maelezo pia yatambulika moja kwa moja na ufikapo hatima utaelekezwa kuwa umefika mwisho. Miisho ya nyimbo inadhihirika kwa uwazi kuliko mianzo. Hata hivyo, kuna mitindo mbalimbali inayotumiwa na hii haimanishi upungufu.

Kwa ufupi mtunzi ametumia ploti imara, inayoshikana na kufululiza usimulizi au maelezo kutoka ubeti wa kwanza hadi mwisho katika nyimbo husika.

4.7 Wakati

Nyakati tatu muhimu zimebainika katika tungo. Nazo ni uliopita, uliopo na ujao. Hata hivyo kuna nyimbo zingine ambazo hazina wakati maalum. Kwa namna msanii anavyoenda nyimbo zake msomaji hujua moja kwa moja jambo linalosimuliwa au elezwa limetokea. Linaendelea kutokea ama litatokea mara nyingi. Mambo yaliyopita husaidia katika kumpa mtu ndoto au njozi ya kutabiria yatakayotokea.

Kwa mfano:

wimbo *kiatu kivue* ubeti 1

*Mungu alinena naye Musa hicho kiatu kivue x 2
Ulichotaka nacho kwa Farao nakwambia kivue.
Mahali hapa ni patakatifu hicho kiatu kivue.*

Mawazo hayo yamewekwa kusimulia historia. Mfano wa pili ni utabiri wa yatakayotokea mfano

wimbo **taabu zangu** ubeti 2

*Haleluyah Nitaketi kwa furaha, nitapumzika kwa Mungu
Nitavikwa mavazi mapya, taji ya ushindi,
Taabu zote na mateso yote hakika zitakoma
Nitaonana na malaika maserafi na makerubi,
tukiimba nyimbo za ushidi haleluyah usifiwe*

Tunahitimisha kuwa tungo zilizomo humu si za wakati mmoja maalum. Ni tungo za nyakati zote.

4.8 Tamathali za Usemi

4.8.1 Sitiari

Katika sura ya tatu tulieleza sitiari kama tamathali ya usemi ambayo hutumiwa kulinganisha vitu viwili tofauti vyenye hulka tofauti pasipo na matumizi ya viungo kama vile “ja” “mithili ya”

‘mfano wa’ ‘kama’ kwa kifupi kitu kimoja (kilinganishwa) hutajwa kuwa kingine (kilinganishi). Kwa sababu fulani (msingi) katika wimbo wa *kiatu kivue* twatambua matumizi ya sitiari katika ubeti wa kwanza..

*Hata leo Mungu anena nasi hicho kiatu kivue
Kiatu ni dhambi uzifanyazo nakwambia kivue
Ukahaba unaoendeleza kando kando ni kiatu kivue
Wivu na masengenyo yanayokuja ni kiatu kivue
Kitakupeleka Jehenamu hicho kiatu kivue.
Usinzi unaoeneza wewe ni kiatu kivue
Kuvalia wake wa wenyewe kutongoza waume
wa wenyewe ni kiatu kivue.*

Hii ni aina ya sitiari fiche ambapo neno “kiatu limetumiwa kulinganisha tabia mbovu ya binadamu kama vile “ukahaba,” unaoendelezwa katika jamii. Vile vile neno “kiatu” latumiwa kama *sitiari dhana* kwa sababu kiatu ni kifaa cha kuvalia mguuni lakini katika muktadha huu neno hili limetumiwa kwa njia tofauti .Uchunguzi umebainisha kuwa sitiari zilizotumiwa ni nyingi za aina tofauti . Aina za sitiari zinazojitokeza hapa ni *sitiari fiche*. *Sitiari pana*, *sitiari dhana*. Imebainika kwamba mtunzi amefanya uteuzi maalum wa sitiari kuambatana na dhamira ya nyimbo zenyewe. Hii inatokana na vilinganishi hivi vinavyohusiana na kuchangizana kikamlifu au kuunda muumano na muwala wa kisemantiki na ambao umesaidia kubaini dhamira ya kidini, ambayo inatokuza dini ya Kikristo.Pamoja na hayo, imedhihirisha kuwa sitiari zinazojitokeza katika nyimbo hizi ni bia. Zinapatikana katika tamaduni zote za ulimwengu na hivyo zinaweza kueleweka kimatini.

4.8.2 Takriri

Takriri ni urudiaji wa silabi neno , mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi za sanaa. Kwa mfano;

Takriri konsonanti

*“Twende tutavikwa taji twende mbinguni”
Yatosha walivyo yatosha walivyokutukana”*

Ambapo “Twe,” “tu” “ta” “twe” – na “ya”,”vyo” “ya” “vyo” vimekaririwa katika mishororo hii miwili ili kuleta ridhimu fulani kimapigo na pia ni vya lazima katika maana iliyokusudiwa kimsamiati.

Usiwe! Usiwe! kama manamba wa matatu

4.8.3 Takriri nomino na nomino

wimbo **manamba** ubeti 1.

Anastacia Mukabwa

*Usiwe ! usiwe! kama manamba wa matatu
anayesema twende kisha anabaki nyuma...
Manamba ni mtu yule jumapili yu kanisani,
lakini matendo yake hayampendezi Mungu
Kupiga dala dala yeye anasema twende,
kisha ikiondoka yeye anabaki nyuma.*

Katika mfano huu maana ya nomino “manamba” imepanuliwa na kusesitizwa na nomino “matatu”

4.8.4 Takiriri ya kitenzi kitenzi

Maji yamenizidi mimi yamenifika nafsini

Walivyokudhulumu yatosha

walivyokupiga karibu uumzike

*(wimbo **nishike mkono** – ubeti 2)*

Ukariri huu wa vitenzi au vipashio kama mizizi ya sentensi inafaa sana katika kusesitiza maana ya kile kinachozungumziwa “*Yamenizidi*” na “*yamenifika*” ina maana ya kukata tamaa, vile vile “walivyokudhulumu” na “walivyokupiga”, na maana ya mateso.

4.8.5 Takriri neno

“*Usiwe! Usiwe! Kama manamba wa matatu* (Wimbo **manamba** ubeti wa pili mshororo wa kwanza)

Eeh! Mungu utukuzwe milele na milele (wimbo **utukuzwe** ubeti wa tatu mshororo wa kwanza).

Mfano wa kwanza unaoyesha msisitizo mkali wa ukataaji kata kata wa tabia ya manamba ambao ni watu wasio na msimamo mfano wa pili unaonyesha hali ya heshima au kujisalimilisha. Si mtindo unaochukiza, una mvutio fulani ambapo katika kila kidato cha ukariri kuna msisitizo fulani wa maana hali ambayo imepanua neno kisematiki.

4.8.6 Takriri kibwagizo.

Mifano hii ni mingi sana na ufuatao utafaa sana katika kutuwesha kutambua namna ulivyotumiwa. wimbo **Heshima**

Wanaokudharao siku moja watakusalimia kwa heshima x 2

Mtunzi amefanya hivyo pale maana inapoelekea kubebwa katika kibwagizo. Pia husaidia katika kuonyesha kuwa bado wimbo ni ule ule .Kuna nyakati ambapo mwimbaji huzungumzia mambo hata matatu tofauti katika shairi moja. Kila kinacholeta ushikamano wa yote hayo katika shairi moja ni ukariri wa kibwagizo.

4.9 Dhihaka

Ni masimulizi yaliyokusudiwa kubeua jambo kisirisiri au maelezo yanayomdunisha mtu. Mfano mzuri upo katika ubeti wa nne wimbo **Heshima** wenye matumizi ya dhihaka.

*“Wanaokudharau siku moja watakusalima kwa heshima x2
Leo wanakuita kikarakosi kesho watakuita bosu.
Wanaokunyima kadi za harusi kesho wataomba shera yako
Maana leo wankupigia kingumi kesho watakupigia saluti*

Msanii ametumia dhihaka kubeua au kudunisha mahasidi. Ametumia usemi unaoficha hisia zake kuhusu tabia hasi inayotekelezwa na watu wenye chuki katika jamii .Kimsingi pana kinaya katika maneno hayo. Ni vigumu katika hali ya kawaida hasidi kumsalimia mwenzake kwa heshima.

4.10 Mdokezo

Msanii Anastacia Mukabwa ametumia tamathali kama njia ya kumwachia msomaji nafasi ya kujaliza mapengo fulani na kumfanya msomaji aashirie mawazo au maarifa Fulani. Kwa mfano,katika wimbo **Manamba** ubeti wa pili, msanii amedokeza kwa kutahadharisha waumini wasiofuata kanuni za Mungu kwamba kuna siku ya hatari ambapo watahukumiwa kulingana na matendo yao. Kutokana na mdokezo huu, msomaji anapati ari ya kutaka kujaliza ni taabu gani itawakumba waumini.

*Siku hiyo ya kutisha siku hiyo ya hatari hukumu itaanza.
Kanisa ni nyumba ya Mungu hakuna cha kusema mimi,
Nilikuwa mchungaji nilikuwa mshiriki au mimi ni mtoto
Matendo yangu yatapimwa ili yakupe kibali utaenda mbinguni
au motoni.*

4.11 Nidaa

Tamathali hii inapotumiwa kwa werevu humwezesha msomaji kupata toni ya uwasilishaji papo hapo. Imetumiwa katika albamu hii kwa wingi na mifano michache ifuatayo imetuwezesha kuthibitisha matumizi yake.

*Ooh baba oh! We, navumilia kwa ajili yako
(Usiwe! Usiwe! Kama manamba wa matatu (**manamba**)
Eeh! Mungu wangu uniokoe mimi wimbo (**Nishike mkono**)*

Matumizi hayo yanatupa sura mbalimbali za tamathali hiyo. Mfano wa kwanza ni ombi baada ya kukosa tumaini, wa pili ni wa ukataaji kata kata, wa tatu ni uvuguvugu (haudhihirishi hisia maalum). Kumetokea toni mbalimbali kutegemea ule mpangilio wa maneno na matini ambayo zimetumiwa. Kwa ufupi ni kuwa, nidaa imetumiwa humo kwa namna inayoibusha hisia fulani na isiyokera msomaji.

4.12 Tashtiti

Ni mtindo unaotumia njia mbalimbali katika kumsawishi msomaji kwa toni inayoziba masafa ujumi na kutathimini moja kwa moja hisia zake. Sifa kuu ya tashtiti ni kuingilia hisia ya ndani ya msomaji na kutawala maamuzi yake kuhusu jambo linalozungumziwa. Kwa mfano wimbo

Taabu zangu.

Ubeti 1 na 2

Taabu zangu zikiisha nitamuona Bwana wangu

*Akinikaribisha kule karibu upumzike eeh.....
Hapo ndipo nyumbani mwako hapa ndipo pahali pako,
hapa ndipo makao yako katibu upumzike.*

*Natazama vidonda vyangu
natazama makovu yangu
yalioumizwa duniani na watu wa ulimwengu
Atachukua kitambaa akinifuta machozi
akisema pole mwanangu Yesu tanikumbatia
Maana kitambo nitapumzika.*

Mifano hiyo ina usawishi wa moja kwa moja kwa msomaji na inaibua hisia za huzuni na pia tumaini kumhusu mwimbaji. Toni katika ubeti wa kwanza ni ya upole huku ya pili ikiguza hisia za ndani kwa msomaji na kumpa faraja.

4.13 Tashihisi

Ufuatao ni mfano mzuri wa tashihisi

Wimbo *Utukuzwe* ubeti 2

*Haya fisi na viumbe, mito naipige makofi
Ndege na waseme amina kubwa wanyama wamuinua
Sifu yaya haya fisi wanabidii mwewe mito naipige makofi.
Ndege na waseme amina,
Baba wanyama wamuinua sifu
Bwana watawala Bwana.*

Kutokana na mfano huo twaona wanyama, na vitu vikiwa na uwezo wa kutenda mambo ya kibinadamu kama kuimba, kupiga makofi na kuzungumza. Katika ulimwengu halisi hayo hayawezekani. Yanawezekana tu katika ulimwengu wa usanii.

Katika matumizi ya mbinu hii, picha inayotokea ni sawa na halisi kama kile hasa kinachopewa sifa hizo. Kwa mfano uhaishaji wa fisi na ndege ni halisi kama binadamu. Mifano hiyo imejenga picha ambazo kisanii zina uwizani unaowafanya wasomaji kuziamini.

4.14 Tasifida

Hii ni hali ya kupunguza ukali au uzito fulani wakati wa mazungumzo, yaani badala ya mhusika kutumia lugha moja kwa moja kutaja jambo au hali fulani, anatumia lugha fiche yenye heshima ili kupunguza makali. Kwa mfano, katika wimbo *manamba*. Ubeti wa nne.

*Enyi watumishi wangu mwasema mmeokoka na huku,
Kando kando mwakata kondoo mkia,
Tabia hiyo itawapeleka motoni.
Ninyi ni kama manamba wanaobaki nyuma,
Badilisha mienendo yenu badilisha tabia zenu,
ili nitakapo rudi niende nanyi milele.*

Kutokana na mfano huu, msanii ametumia maneno kwa njia fiche na kuondoa ukali kwa kutotaja moja kwa moja tabia ya kujamiiana, ametumia maneno kama: *mwakata kondoo mkia* kulejelea ukahaba unaofanywa na viongozi wa kidini dhidi ya waumini wao. Mbinu hii imetumika kijazanda na kuficha ukweli.

SURA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunatoa hitimisho la utafiti huu, tumefanya hivyo kwa kutoa muhtasari wa yale tuliyoyatekeleza na kuyaiibua katika uchunguzi huu. Tumelejelea madhumuni ya utafiti na kupima nadharia tete za utafiti huu, matatizo tuliyokumbana nayo, hatimaye tukatoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

5.1 Kuhusu madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza matumizi ya fani katika nyimbo za Anastacia Mukabwa kisha kujadili ufaafu wa fani zilizotumiwa kuwasilisha ujumbe katika alamu yake *kiatu kivue*, huku tukiongozwa na nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Nadharia hii imetusaidia kuchanganua vipengele mbalimbali vya fani.

5.2 Muhtasari wa matokeo

Kitaaluma, utafiti huu umefanikiwa kujibu nadharia tete zilizo rodheshwa. Tulitaka kuthibitisha kwamba viungo vya fani vimeingiliana vyema katika utanzu wa fasihi simulizi, vile vile tamathali za usemi zimechangia pakubwa katika nyimbo za Anastacia Mukabwa. Kupitia matokeo ya utafiti wetu tumeona kwamba nadharia yetu hii ina mashiko. Tumeona jinsi msanii ametumia fani ambazo tumeshapitia kuwasilisha ujumbe wake. fani zimetumika kufungamanisha kazi ikawa na mtiririko mzuri wa uwasilishaji wa ujumbe.

Pia fani hizi zimetumika kutia ladha kazi hii na kumvutia msomaji aendelee kusoma. Vile vile tumeona ya kwamba msamiati umeteuliwa na kutumika kwa njia mwafaka. Vipengele vya ploti,

mandhari, toni, na wakati vimetumika vizuri na matukio yametendeka katika mandhari ya kawaida ambayo yanaeleweka na mwanadamu wa kawaida. Vile vile wahusika ambao wametumika ni wa kawaida.

Sura ya pili tulishughulikia nyimbo mbalimbali na umuhimu wake kwa jumla katika jamii ya Afrika. Nyimbo kama sehemu muhimu ya jamii hutoa picha ya utamaduni husika. Kwani kile kipengele cha maisha kinachohusu jamii hiyo hujitokeza katika nyimbo mbalimbali. Kwa hivyo kupitia nyimbo jamii fulani inaweza kusawiriwa kimila, miiko, na utamaduni wake kwa jumla. Nyimbo basi huimbwa kuangazia mazuri ili yaweze kuigwa na kuhifadhiwa na vile vile huimbwa kwa madhumuni ya kukashifu mabaya ili yarekebishwe na pia yasiendelezwe na kizazi cha baadaye. Ukweli wa kauli hii tumepata kwenye maudhui ya nyimbo za Anastacia Mukabwa.

Katika sura ya tatu, tulishughulikia maana ya fani na vipengele vya kifani tukiongozwa na nadharia ya uhakiki. Tulichukua maoni ya wataalamu mbali mbali walioeleza maana ya fani ili tupate mwongozo wa kujadili fani. Tilitambua kwamba fani ni umbo, ufundi, umbo au muundo wa kazi ya sanaa. Kwa ufupi ni kuwa fani ni mbinu za kisanaa ambazo hutumiwa katika kuwasilisha ujumbe au maudhui. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya lugha, mandhari, wakati, wahusika, na ploti ambavyo huweka wazi mtazamo wa msanii katika kuyaza toni ya kazi. Tumeona pia fani ina uwezo mkubwa wa kumtawala kihemshi msomaji. Hii inategemea namna msanii alivyoitumia lugha, alivyowaweka wahusika wake na kuwaumba, aina ya mandhari ambamo hutumiwa na muktadha wake kuhusu kazi na wasomaji wa fasihi simulizi.

Katika sura ya nne, tumeona kuwa msanii ametumia fani yenye mwelekeo mzuri ambao unafungamana na udhabiti wa dhamira alizozilenga msanii. Msanii Anastacia Mukabwa ametumia fani kwa namna ambayo inamruhusu mhakiki kuvichanganua na kuvihakiki vipengele vyake katika kutathmini mchango wa kila mojawapo kabla ya kuangalia kimantiki uhusiano baina yao. Ametumia fani kwa namna ambayo inaruhusu uwezekano huo, na ni kwa sababu hiyo tuliangalia kila kimojawapo kivyake na wakati mwingine kuangalia uhusiano wao.

Kwa mfano, msamiati ulioteuliwa umejikita katika sajili ya kidini. Msanii ameteua msamiati unaoibua toni ya huzuni, masikitiko, chuki dhidi ya shetani, huruma na furaha. Ametumia msamiati wenye uwezo wa kunasa makini ya msomaji kiasi kwamba anawashirikisha vilivyo ujuzi wa kutumia msamiati ; kwa njia hii umemwezesha kuzua mazingira yasiyoonekana kuwa halisi. Mtindo wa kueleza mambo halisi kitafsili unaipatia kazi hii mvuto kwa msomaji. Pia mwimbaji ametumia tamathali mbalimbali kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wake. Ametumia chuku kuisitiza kiwango cha matatizo yanayomkumba binadamu katika wimbo **“Taabu Zangu”** na nyimbo zinginezo. Pia ametumia tamathali zingine kama vile tashbihi, na sitiari ambazo zinazua ulinganishi wa picha na hali ya kawaida zinazozalisha uelewekaji wa kazi yake. Ni bayana kwamba msanii ametumia mbinu ya takriri kwa ufanisi kiasi kwamba aina mbalimbali za takriri zimejitokeza. Hizi ni takriri irabu na takriri neno. Mbinu ya takriri hutumika kuisitiza wazo fulani, Kipengele cha wahusika pia kimetumika vizuri. Mtunzi amewatumia wahusika wa kawaida na vitu vinavyofahamika kama vile viatu ili kuendeleza ujumbe .Wakati ambao ni muhimu sana katika kuhusishwa na matukio simulizi umetumiwa kwa namna ambayo unapambanuka kwa urahisi. Umetumiwa kwa njia ambayo imetuwezesha kupata na kutambua matumizi ya njozi katika fungu.

Ploti nayo imetokea vizuri ambapo maumbo yake ya msago au moja kwa moja au fululizi na ya taharuki yamethibitika katika matumizi. Ni aina ya ploti iliyozipa nyimbo vichwa, miili na hitimisho.

Mwisho kuna mdhihiriko wa toni ambayo ni zao la namna uwasilishi unavyofanywa, unahusisha nani? katika mazingira yapi? Katika wakati upi. Tumeona pia toni ni matokeo ya ushirikiano wa vipengele vyote vya fani.

Ni kwa sababu hizo mbalimbali tumehitimisha kuwa msanii ametumia fani nzuri ambayo imetekeleza uamili wake kwa namna inayodhibiti na kutimiza malengo kuu ya kisanii na uwasilishi kwa ufundi mkubwa.

5.3 Changamoto tulizokubana nazo katika utafiti

Utafiti wetu ulifanywa maktabani na nyanjani. Sampuli yetu ilikuwa sampuli lengwa. Tulizuru mji wa Nairobi hasa kanisa la LORD'S MIRACLE kupata habari toshelevu kumhusu Anastacia Mukabwa. Waumini wengine walikiri kujua nyimbo zote za mwimbaji huyu lakini hatukupata historia yake. Jambo la kusikitisha ni kwamba wengi wa wachuuzi wanaouza kanda za nyimbo za Anastacia Mukabwa wamenakili nyimbo hizo kinyume cha sheria hivyo ilikuwa vigumu kupata albamu iliyoidhinishwa na mwimbaji mwenyewe. Tulitembelea kituo cha redio cha Milele F.M ambapo tulipata nakala nadhifu ambayo ilitusaidia kusikiza na kunakili nyimbo zetu. Vile vile tulipata historia ya mwimbaji Anastacia Mukabwa.

5.4 Pendekezo

Maudhui ni kiunzi cha fani kama tulivyotangulia kusema hapo mwanzoni. Tuligusia maudhui pindi tu ilipohitajika tulipokuwa tukifafanua vipengele mbalimbali vya fani. Kwa hivyo,

tungependekeza wahakiki wa baadaye, wahakiki maudhui katika albamu hii na nyimbo zingine za Anastacia Mukabwa. Sisi tumetumia nadharia ya umitindo, tungependekeza wahakiki wa baadaye watumie nadharia ya maadili, au nadharia nyingine mwafaka. Watafiti wakishughulikia maswala haya bila shaka watachangia katika ukuaji wa fasihi simulizi ya Kiswahili.

Marejeleo

Barry, P. (2002). *Structuralism: Beginning theory: An introduction to Literary and Cultural theory*. Manchester, Manchester University Press.

Catman, S. (1967). *Literary style – A symposium*, New York , US.

Cuddon. J.A. (1977). *A Dictionary of literary terms* London, Andre Deutch Ltd.

Hillary, P. (1973). “*Meaning and reference,*” *Journal of Philosophy Department of Linguistics*,
Staford. Stanford University Press.

Halman, C. na Harmon, .W. (1986). *A handbook to Literature* New York. Macmillan.

Jones, M. R. (1987): *Dynamic Pattern Structure in Music: Recent theory and research: In Perception & Psychophysics*. Vol.41/6,pp.621-634

Kazungu, K. (1982) *Deviation and fore groudng in chosen Swahili Literary text*, Tasnifu ya
MA Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kimani N. Na Chimerah, K. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi* ,Nairobi: Jomo Kenyatta
Foundation.

Kirumbi, P. (1975) *Misingi ya Fasihi Simulizi* . Nairobi .Shungwaga Publishers.

Kuhenga, C , (1977). *Tamathali za Usemi*. Dar es salam East Africa Literature Bureau

Leech, G. Na Short , M.A. (1981). *Style in fiction. An introductions to English fictional prose*,
London: Longman.

Mattteru, J. (1981). *Fasihi Simulizi na Uandishi makala ya semina ya waandishi wa Kiswahili*
Dar-es-Salaam.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard textbook group and Publishing

Msokile, M. (1993). “*Misingi ya Uhakiki wa Fasihi .*” Nairobi; E.A.E.P Ltd.

Nkong’e. M. (2008). *Literacy study of songs of Joseph Kamaru. Theme and styles*.
MA Chuo Kikuu cha Nairobi.

Senkoro, F.E.M.K, (1982), *Fasihi ya Kiswahili* Dar-es-salaam. Press and publicity centre.

Simpson, P. (2004) . *Stylistics*. A resource Book for Students., London Routledge.

Timammy, R. (2002). *Swahili women’s wedding songs: A stylistic Analysis* Tasnifu ya Ph.D
Chuo Kikuu cha Nairobi.

Tuki (1981) *Kamusi ya Kiswahili sanifu*:London Oxford

Wamitila, K.W. (2008): *Kanzi ya Fasihi (1): Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide-Muwa Publishers.

----- (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*, Focus publications Ltd., Nairobi.

Weseh, E. (2005). *Uhakiki wa Kifani katika Utenzi wa Siri li Asirali na Mwana Fatuma*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Hajichapishwa).

Yalwala, P. (1991). *Maudhui katika nyimbo za John Mwale* “Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).

VIAMBATISHO

KIATU KIVUE

Anastacia Mukabwa

*Mungu alinena naye Musa hicho kiatu kivue x 2
Ulichotaka nacho kwa Farao nakwambia kivue.
Mahali hapa ni patakatifu hicho kiatu kivue.*

*Musa hicho kiato kivue x2
Nataka ninene nawe kivue
Nataka nikutumie kivue
Nataka nikuinue kivue
Nataka nikubariki kivue
Watu wangu waagama taifa langu la Israeli kivue
Watu wangu wanasononeka watu wangu wanateseka kivue
Nataka nikutume wewe ukaokoe taifa langu la Israeli Kivue.*

*Hata leo Mungu anena nasi hicho kiatu kivue
Kiatu ni dhambi uzifanyazo nakwambia kivue.
Ukahaba unaoendeleza kando kando ni kiatu kivue.
Wivu au masengeyo yanayokuja ni kiatu kivue
Kitakupeleka jehenamu hich kiatu kivue
Uzinzi unaoeneza wewe ni kiatu kivue
Kuvalia wake wa wenyewe kutongoza waume wa wenyewe
ni kiatu kivue.*

*Nataka ninene nawe maana ninakupenda kivue
Nataka ninene nawe ili nikuokoe kivue
Mimi sitaki uangamie mimi sitaki upotee kivue
Mimi sitaki uangamie maana mimi ninakujali kivue
Mimi Mungu ni wa neema kivue
Mimi Mungu ni wa upendo kivue
Ukitaka Mungu akubariki lazima kiatu ukivue
Ukitaka kuinuliwa ni lazima kiatu ukivue
Wivu uliyo nao wewe ni lazima kiatu ukivue
Hutaki kuona wenzako kama wakiinuliwa wewe Kivue*

*Hutaki kumwona mwenzako akiwa amependeza kivue
Hutaki kumwona mwenzako akiwa ako Smart kivue
Tabia uliyonayo mama na kwambia kivue
hutaki kuona ndoa ya mwenzako mume na mke wakicheka kivue
Tabia uliyo nayo mama kivue,
nakwambia badilika Kivue,*

Hutaki kuona huduma ya mwenzako ikisonga kivue

*Mbele kivue, hebu kivue
Jamani kivue kiatu cha nyumba ndogo kivue
Kiatu cha ulevi , kiatu cha uzinzi kiatu cha kivue*

*Ooh ooh ooh kivue kiatu kiatu kivue kivue
(Mungu anena nawe hicho kiatu kivue z2)
Waliowadhamini waume wa wenyewe iwe mwisho Kivue
Kualia vitumbua mume wa wenzio iwe mwisho kivue
Kupaka wanja kwa mume wa mwenzio iwe mwisho Kivue
Nataka nikupe mumeo nataka kikupe nyumba yako nataka kivue
Nikuinue..... nataka nikuinue mume wako kivue
Niinue nyumba yako kivue,
niinue mke wako nikubariki kivue,
Mchumba kivue kiatu cha nyumba ndogo kivue
Mungu anasema na wewe hicho kiatu kivue
aah aaah aah kivue.*

Heshima

Anastacia Mukabwa

*Wanaokudharao siku moja watakusalimia kwa heshima
Mateso yako ni ya muda Mungu akuandalia ushuhuda
Daudi alikuwa mchungu kondoo,
Mungu akamuinua akawa mfalme
Leo unaitwa omba omba kesho utaitwa mbarikiwa
Licha ya ukutembea kwa miguu kesho utaendesha gari
Nasema watakusalima kwa heshima x2
Hasa ukiinuliwa watakusalimia kwa heshima
Watakuita mheshimiwa watakusalima kwa heshima
Hasa ukikumbukwa watakusalimia kwa heshima*

*Wanaosema hautaolewa watashuhudia ndoa yako
Mara utakapo valishwa pete watapatwa na kugugumizi,
Wanaosema wewe ni tasa wataona ukinyonyesha
Mungu aliyemkumbuka Sarah hata wewe utakumbukwa.
Nasema watakusalimia kwa heshima x2
Wakati wako wakuinuliwa ukifika watakusalimia kwa heshima
Wakati wangu wa kubarikiwa ukifika watakusalimia kwa heshima x2
Wakati wako wa kukumbukwa ukifika watakusalimia kwa heshima x2*

*Kwa kuwa Mungu ni Ebenzar hata sasa yupo msaada wetu wa karibu
Mwite ataitiikia jifunze kuwa na subira atubarikiwa sana
Siku usiodhani maana atakuinua
wanaokudharao siku moja watakusalimia kwa heshima.
Leo wanakuita kikarakosi kesho watakuita bosi
Wanaokunyima kadi za harusi kesho wataomba Shera lako.
Maana leo wanakupigia kingumi kesho watakupigia saluti
Watakusalimai kwa heshima x2
Waliokuona jelani kesho watakukuta ofisini
Watakusalima kwa heshima x2
Watakupigia saluti watakusalimia kwa heshima x2*

Manamba

Anastacia Mukabwa

*Usiwe ! usiwe! kama manamba wa matatu
anayesema twende kisha anabaki nyuma...
Manamba ni mtu yule jumapili yu kanisani,
lakini matendo yake hayampendezi Mungu
Kupiga dala dala yeye anasema twende,
kisha ikiondoka yeye anabaki nyuma.*

*Siku hiyo ya kutisha siku hiyo ya hatari hukumu itaanza.
Kanisa ni nyumba ya Mungu hakuna cha kusema mimi,
Nilikuwa mchungaji nilikuwa mshiriki au mimi ni mtoto
Matendo yangu yatapimwa ili yakupe kibali utaenda mbinguni au motoni.*

*Mwendapo kanisani hamwendi kuniabudu
Mwaenda mjulikane muone jamaa wa kanisa
Tatizo liwapatapo kanisa liwasaidie
lakini moyoni hamkuweka Mungu wenu,
Badilisheni mienendo yenu
Badilisheni tabia zako ili nitakapo rudi niende nanyi milele mbinguni.*

*Enyi watumishi wangu mwasema mumeokoka
Na huku kando kando mwakata kondoo mikia
tabia hiyo Itawapeleka motoni nyinyi ni kama manamba wanaobaki
nyuma. Badilisha mienendo yenu badilisha tabia zenu
ili nitakapo rudi niende nanyi milele.*

*Kaza mwendo twendee ... ili tufike mbinguni enyi wachungaji
Twende wainjilisti twende, waimbaji twende tufike mbinguni.
Mbinguni tunagojewa twende tutapanguzwa machozi .
Twende tutavikwa taji twende mbinguni
Usitazame nyuma ya dunia yanapita twende kaza mwendo twende tufike
mbinguni.
Tunangojewa twende usitazame nyuma twende, nyuma kuna hatari tufike
mbinguni.
Tunangojewa twende tukisalimiwa na heshima
sote twende pale tutalakiwa twende tufike mbinguni
kaza mwendo twende kaza mwendo twende ili tufike nyumbani.*

Utukuzwe

*Eeeh! Mungu utukuzwe milele na milele,
tena uinuliwe katika mataifa yote x2
Eeeh! Mungu utukuzwe milele na milele
Eeh! Mungu utukuzwe milele na milele.
Eeeh ! Mungu uinuliwe milele na milele,
tena uhindimiwe katika mataifa yote jina lako litukuzwe
Uliupiga mwamba maji yakabubujika katika kila janga,
walipokutana na adui wewe uliwapigania
ndipo uliwafikisha kule kanani x2
Usifiwe oiye ... utukuzwe uinuliwe usifiwe baba
Utukufu ni wako hadi milele usifiwe
Utukuzwe usifiwe milele hadi milele*

*Haya fisi viumbe na mito naipige makofi
Ndege na waseme amina kubwa wanyama wamuinua
Fisi wanabidii mwewe mito na ipige makofi,
ndege nawaseme amina baba,
wanyama sifu bwana watawala bwana.*

*Heshima na enzi ni vya bwana utukufu na nguvu ni vya
Bwana umeketi mkono wenye nguvu maana unatawala
Wewe bwana. Wewe uliupiga mwamba maji yake
Bubujika ulipokumbana na adui wewe uliwapigania
Wakafika kule kanani mwisho x2*

*Usifiwe oiye! Utukuzwe uinuliwe usifiwe baba
Utukufu ni wako milele hadi milele usifiwe utukuzwe
Usifiwe milele hadi milele.
Heshima ni yako milele na milele
utukufu ni wako milele na milele.*

Wimbo taabu zangu

*Taabu zangu zikiisha nitamwone Bwana wangu
Akinikaribisha kule karibu upumzike eeh...,
Hapa ndipo nyumbani mwako, hapa ndipo pahali pako
Hapa ndipo makao yako karibu upumzike...*

*Haleluyah Nitaketi kwa furaha, nitapumzika kwa Mungu
Nitavikwa mavazi mapya, taji ya ushindi,
Taabu zote na mateso yote hakika zitakoma
Nitaonana na malaika maserafi na makerubi,
Tukiimba nyimbo za ushidi haleluyah usifiwe*

*Naona mbingu zimefunguka na Yesu yu mkono wangu
Akiniita, kwa upole na macho yenye huruma.
Natazama vindonda vyangu, natazama makovu yangu,
yalioumizwa duniani na watu wa ulimwengu.*

*Yatosha walivyokuonea yatosha yalivyosemea karibu upumzike
Yatosha walivyokuonea yatosha walivyokudhulumu
Yatosha walivyokupiga karibu upumzike
Haleluya mateso yangu yakiisha nitauona uso wa Mungu
Nitamwona Yesu niligepigwa kwa ajili yake.
Yatosha walivyokuonea yatosha walivyokudhulumu,
Yatosha walivyokupiga karibu upumzike*

Zinzilela

Anastacia Mukabwa

Zinzilela wakata na mule zizi lela zizi lela

Ehh bwana nakuinua nikikumbuke

Ulikonitoa kwenye maisha ya aibu na kunifanya wa dhamani x2

Kama si wewe ningekua wapi sisi wewe

Ningelitwa nani ningelikua ni

Nimekufa kwenye shimo la uharibifu x2

Yeeh baba yeeh

(ni wengi niliowajua wenye mapesa na matajiri

Wenye majumba ya kifahari lakini leo hawapo tena x2)

Lakini mimi wanilinda bure

(si kwamba nimetenda mema baba bali ni kwa

Neema yako ndio maana mimi naishi x2)

Wacha nikutukuze wee wewe

(Siwezi kukulipa baba kwa yale umenitendea

Bali naomba moyoni mwangu nipe moyo wa

Kukupenda x2)

(Niondolee kiburi baba nipe moyo

Mnyenyekevu ili kikuishie wewe siku zote za maisha yangu x2)